**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI**

# HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI

**MHESHIMIWA**
**RAHMA KASSIM ALI (MBM)**

**KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

**MEI, 2024**

# UONGOZI WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI ZANZIBAR



Mhe. Rahma Kassim Ali
Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi



Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma
Naibu Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi



Ndg. Khadija Khamis Rajab
Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi



Ndg. Mhaza Gharib Juma
Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi



Ndg. Bakari Ali Bakari
Afisa Mdhamini



Ndg. Khamisuu H. Moh'd
Mkurugenzi Uendeshaji na Utumishi

Mkurugenzi Mipango, Sera na Utafiti



Ndg. Hannat H. Bakar
Mkurugenzi Maendeleo ya Makaazi



Dkt. Abdul-Nasser Hikmany
Katibu Mtendaji Kamisheni Ardhi



Ndg. Mwanaisha A. Said
Mkurugenzi Mkuu Shirika la Nyumba



Ndg. Is-haka A. Khamis
Mwenyekiti Mahakama ya Ardhi



FRV. Tahir M. Omar
Mthamini Mkuu wa Serikali

## YALIYOMO

UONGOZI WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI – ZANZIBAR ....................i
YALIYOMO .................... ii
ORODHA YA VIAMBATANISHO ....................iv
VIFUPISHO VYA MANENO ....................vi
UTANGULIZI ....................1
MUUNDO WA WIZARA ....................3
MAJUKUMU YA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI ....................4
MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 ....................5
MUHTASARI WA MAPATO ....................5
MUHTASARI WA MATUMIZI ....................6
UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA MWELEKEO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 ....................7
PROGRAMU KUU PN0201: UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI ....................7
PROGRAMU NDOGO SN020101: URATIBU WA MIPANGO, SERA NA UTAFITI ....................8
PROGRAMU NDOGO SN020102: UTAWALA NA UENDESHAJI ....................14
PROGRAMU NDOGO SN020103:URATIBU WA SHUGHULI ZA WIZARA PEMBA ....................18
PROGRAMU KUU PN0202: USIMAMIZI WA ARDHI ....................21

PROGRAMU NDOGO SN020201: USIMAMIZI WA ARDHI ........................................................................ 22
HN02020108: UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI – MAHAKAMA YA ARDHI ................................ 22
HN02020107: KUSIMAMIA NA KUIDHINISHA RIPOTI ZA UTHAMINI – OFISI YA MTHAMINI MKUU WA SERIKALI ................................................................ 24
HN02020101: UPANGAJI NA USIMAMIZI WA ARDHI – KAMISHENI YA ARDHI ................................ 27
PROGRAMU KUU PN0203: MAENDELEO YA MAKAAZI ................................................................ 33
PROGRAMU NDOGO SN020301: MAENDELEO YA MAKAAZI................................................................. 34
HUDUMA HN02030102 USAJILI WA MAJENGO NA JUMUIYA YA KONDOMINIO........................................... 34
HN02030105 UTATUZI WA MIGOGORO KWA WAPANGAJI WA NYUMBA – BODI YA KUDHIBITI KODI ZA NYUMBA.......................................................... 38
SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR.............................. 39
MWELEKEO WA MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025. .................................... 45
HITIMISHO............................................................... 47

# ORODHA YA VIAMBATANISHO

**Kiambatanisho Nambari 1(a):** Muhtasari wa ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ................. 52 – 53

**Kiambatanisho Nambari 1(b):** Muhtasari wa Matumizi ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ........................ 54

**Kiambatanisho Nambari 1(c):** Mchanganuo wa Makadirio ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ......................... 55

**Kiambatanisho Nambari 1(d):** Mchanganuo wa Makadirio ya Bajeti kwa kipindi cha Miezi Tisa (Julai 2023- Machi 2024) .......................................... 56

**Kiambatanisho Nambari 1(e):** Muhtasari wa matumizi ya Bajeti kwa programu kuu na ndogo kwa kipindi cha Julai 2023 – Machi 2024......57 -58

**Kiambatanisho Nambari 2:** Maeneo yaliyofanyiwa ukaguzi wa ujenzi .......................... 59

**Kiambatanisho Nambar 3:** Idadi ya Wafanyakazi waliopatiwa Likizo na Stahiki .......................................... 60

**Kiambatanisho Nambari 4(a)**: Mafunzo ya muda mfupi kwa Wafanyakazi wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ........................ 61

**Kiambatanisho Nambari 4(b):** Mafunzo ya muda mrefu kwa Wafanyakazi wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi 2023/2024... 62– 64

**Kiambatanisho Nambari 5**: Mashauri Mapya yaliyopokelewa, yanayoendelea na yaliotolewa uamuzi .... 65

**Kiambatanisho Nambari 6(a):** Makadirio ya Ukusanyaji wa Mapato kwa Fungu la Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ........................ 66

**Kiambatanisho Nambari 6(b):** Makadirio ya Fedha za Matumizikwa Fungu la Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ........................ 67

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| BPI | Bank of Philipines Islands (Benki ya Visiwa vya Ufilipino) |
| COLA | Commission for Lands (Kamisheni ya Ardhi). |
| DCU | Development Control Unit (Kamati ya Usimamizi na Udhibiti wa Ujenzi) |
| EPZ | Export Process Zone |
| ILMIS | Intergrated Land Manangement Information System (Mfumo Shirikishi wa Taarifa za Ardhi) |
| ZHC | Zanzibar Housing Corporation (Shirika la Nyumba Zanzibar) |
| ZIPA | Zanzibar Investment Promotion Authority (Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar |
| ZUPIN | Zanzibar Unique Plot Identification Number |

**HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO MAKAAZI MHESHIMIWA RAHMA KASSIM ALI (MBM) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR.**

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**; Kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

2. **Mheshimiwa Spika**; Awali ya yote, naomba nichukue nafasi hii adhimu kumshukuru Allah (S.W) kwa kutuwezesha kufika mbele ya Baraza lako tukiwa katika hali ya uzima, salama, amani na utulivu wa hali ya juu katika uwasilishaji wa Hotuba ya Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Vilevile, niendelee kumshukuru Allah (S.W) kwa kutujaalia uwezo na nguvu za kutekeleza Majukumu tuliyojipangia katika kujenga Nchi yetu pamoja na kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

3. **Mheshimiwa Spika**; Kwa niaba ya Viongozi na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi tunampongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyoendelea kuiongoza Nchi yetu, kwa kufanya kazi nzuri ya kuwaletea Maendeleo Wananchi wa Tanzania kwa ujumla, kwa kuzingatia misingi ya haki, usawa na uwajibikaji pamoja na kusimamia na kutekeleza

kwa vitendo Miongozo na Sera za Nchi ikiwemo Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 – 2025. Namuomba Mwenyezi Mungu azidi kumsimamia katika kuendelea kutekeleza majukumu yake hayo. Vile vile, tunatoa pole kwa Wananchi wote waliopata mitihani ya mafuriko na upepo mkali katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu na namuomba Allah (S.W) awape faraja.

4. **Mheshimiwa Spika**; Kipekee kabisa, namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa namna anavyowatumikia Wananchi wa Zanzibar na kuwaletea maendeleo katika Nyanja za kijamii, kisiasa na kiuchumi. Sote ni mashuhuda wa nchi inavyopiga hatua za maendeleo ikiwemo ujenzi wa Makaazi bora, Barabara, Skuli, Vituo vya Afya na Miundombinu mengine Unguja na Pemba. Pia, namshukuru kwa kuendelea kuniamini kuiongoza Wizara hii pamoja na kusimamia Misingi ya uzingatiaji wa jinsia kwani safu za juu za Wizara hii zote zinaongozwa na kinamama. Namuomba Mwenyezi Mungu amzidishie upeo, busara na hekima ili azidi kutuletea Maendeleo katika Nchi yetu.

5. **Mheshimiwa Spika**; Niwapongeze kwa dhati Mheshimiwa Othman Masoud Othman Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa jinsi wanavyomsaidia Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kusimamia utekelezaji wa Mipango, Ilani na Sera za nchi kwa lengo la kuleta Maendeleo kwa Wananchi na Nchi kwa ujumla.

6. **Mheshimiwa Spika**; Shukrani ziende kwako Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa maoni, michango na maelekezo wanayotoa kwa Wizara ili iweze kutekeleza majukumu yake vyema. Pia, kwa dhati kabisa nampongeza Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati, Makamo Mwenyekiti, Wajumbe na Wasaidizi wake wote kwa kuongoza vyema Kamati hiyo kwa hekima na busara katika kuhakikisha kazi za Serikali zinatekelezwa kwa ufanisi mkubwa. Nawashukuru nyote kwa ushirikiano wa hali ya juu mnaoipatia Wizara, ushauri na maelekezo mbali mbali ambayo yamekua chachu ya kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya kila siku.

## MUUNDO WA WIZARA

7. **Mheshimiwa Spika**; Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi inaundwa na Sekta mbili kuu; Sekta ya Ardhi na Sekta ya Makaazi na imejumuisha Idara Tatu (03) ambazo ni Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango Sera na Utafiti na Idara ya Maendeleo ya Makaazi pamoja na Ofisi Kuu Pemba. Aidha, Wizara ina Taasisi tatu (03) na Shirika moja ambazo ni Kamisheni ya Ardhi (COLA), Mahakama ya Ardhi, Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali na Shirika la Nyumba Zanzibar (ZHC). Vilevile, Wizara ina Bodi Tatu ambazo ni; Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba, Bodi ya Kamisheni ya Ardhi na Bodi ya Shirika la Nyumba.

## MAJUKUMU YA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI.

8. **Mheshimiwa Spika;** Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi inatekeleza majukumu makuu yafuatayo:-

i. Kutunga na Kusimamia Utekelezaji wa Sera za Kisekta na Sheria zinazohusiana na Ardhi, Nyumba na Makaazi;
ii. Kushajihisha na Kusimamia Upatikanaji wa Makaazi Bora na Nafuu kwa Wananchi;
iii. Kusimamia Utambuzi, Usajili, Umiliki wa Ardhi na Shughuli za Ujenzi Nchini;
iv. Kufanya Tafiti, Ufuatiliaji na Tathmini za Shughuli zinazohusiana na Sekta ya Ardhi, Nyumba na Makaazi;
v. Kutayarisha na Kusimamia Utekelezaji wa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi Mijini na Vijijini;
vi. Kusimamia Rasilimali Watu, Fedha na Rasilimali nyenginezo za Wizara; na
vii. Kuimarisha Mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa yanayohusiana na Sekta ya Ardhi, Nyumba na Makaazi.

**9.** **Mheshimiwa Spika**; Baada ya utangulizi huo, naomba sasa uniruhusu kuelezea utekelezaji wa Kazi za Kawaida na za Maendeleo za Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na mwelekeo wa Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

## MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

## MUHTASARI WA MAPATO

10. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi ilipangiwa kukusanya jumla ya **TZS 7,505,603,000** kutoka vyanzo vyake vya Mapato ambapo **TZS 4,318,713,000** kutoka katika vianzio vilivyomo ndani ya Fungu la Wizara (Ada ya Mahakama, Usajili wa Kondominio, Vibali vya Ujenzi na Ada ya Uthamini); **TZS 2,750,890,000** kwa ajili ya Mapato yanayotokana na vianzio vilivyomo ndani ya Fungu la Kamisheni ya Ardhi (Nyaraka za Ardhi, Muongozo wa Matumizi ya Ardhi, Upimaji na Ramani, Usajili wa Ardhi, Uhaulishaji na Ada ya Uthamini) na **TZS 436,000,000** kutoka vyanzo vya Taasisi ya Wakala wa Majengo Zanzibar (Ukodishwaji wa Majengo ya Serikali, Ada ya Ushauri elekezi pamoja na Mapato ya Kazi za Biashara).

11. **Mheshmiwa Spika**; **TZS 436,000,000** zimehamishiwa katika fungu la P01 la Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Baada ya Uhamisho wa Taasisi ya Wakala wa Majengo. Hivyo, Wizara imebakiwa na Jumla ya **TZS 7,069,603,000** za kukusanya.

12. **Mheshmiwa Spika**; Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **TZS 7,015,033,546** zimekusanywa sawa na **asilimia 99** ya makadirio ya makusanyo ya Miezi Tisa na **asilimia 93** ya makadirio ya Mwaka. **Kiambatanisho nambari 1 (a)** kinafafanua.

## MUHTASARI WA MATUMIZI

13. **Mheshmiwa Spika**; Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS 17,009,200,000** kati ya fedha hizo, jumla ya **TZS 1,012,620,000** kutoka Taasisi ya Wakala wa Majengo, Bodi ya Wahandisi na Bodi ya Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo ambapo zimehamishiwa katika fungu la P01 – Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi. Hivyo, Wizara imebakiwa na **TZS 15,996,580,000**. Kati ya hizo **TZS 7,120,224,000** Mishahara; **TZS 3,340,281,000** Matumizi ya Kawaida; **TZS 986,075,000** Ruzuku na **TZS 4,550,000,000** kazi za Maendeleo.

14. **Mheshmiwa Spika**; Kwa kipindi cha Miezi Tisa, Wizara ilikadiria kutumia jumla ya **TZS 12,943,504,373** ambapo **TZS 5,339,626,317** Mishahara, **TZS 2,560,541,086** Matumizi ya kawaida, **TZS 4,082,400,000** Kazi za Maendeleo na **TZS 960,936,970** Ruzuku.

15. **Mheshimiwa Spika**; Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **TZS 6,254,344,896 (TZS 4,550,921,975 Mishahara, TZS 273,196,000** Ruzuku na **TZS 1,430,226,921** Matumizi ya Kawaida) zimepatikana ambapo sawa na **asilimia 48** kwa Miezi Tisa na **asilimia 39** kwa mwaka. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo hakuna fedha iliyopatikana. **Kiambatanisho nambari 1(b), (c), (d) na (e)** vinafafanua.

## UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA MWELEKEO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

16. **Mheshimiwa Spika**; Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara imetekeleza majukumu yake kupitia Programu Kuu tatu ambazo ni Programu PN0201: Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, Programu PN0202: Usimamizi wa Ardhi na Programu PN0203: Maendeleo ya Makaazi.

## PROGRAMU KUU PN0201: UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI

**17.** **Mheshimiwa Spika**; Programu Kuu PN0201 ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi ina jukumu la kuimarisha uratibu katika utekelezaji wa kazi za Wizara ambayo inajumuisha Programu ndogo tatu ambazo ni Programu ndogo SN020101 ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti; Programu Ndogo SN020102 ya Uendeshaji na Utumishi na Programu Ndogo ya SN020103 ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba.

**18.** **Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu Kuu PN0201 ilikadiriwa kukusanya Jumla ya **TZS 1,504,000,000** kutokana na vyanzo vyake vya mapato na **TZS 1,124,560,000** ilikadiria kukusanya kwa Miezi Tisa. Hadi kufikia Machi, 2024, fedha zilizokusanywa **TZS 461,965,801** sawa na **asilimia 41** kwa Miezi Tisa na **asilimia 31** kwa Mwaka.

19. **Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu Kuu PN0201 ilikadiriwa kutumia jumla ya **TZS 4,947,496,000** (**TZS 3,736,896,000** Mishahara na **TZS 1,210,600,000** Matumizi ya Kawaida) na **TZS 3,776,667,977** (**TZS 2,802,672,777** Mishahara na **TZS 973,995,200** Matumizi ya Kawaida) kwa Miezi Tisa. Hadi kufikia Machi, 2024, Jumla ya **TZS 2,468,645,930** (**TZS 2,056,704,572** Mishahara na **TZS 411,941,358** Matumizi ya kawaida) zilipatikana sawa na **asilimia 63** kwa Miezi Tisa na **asilimia 50** kwa Mwaka.

20. **Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu kuu kupitia Programu ndogo tatu zimetekeleza shughuli zifuatazo:-

**PROGRAMU NDOGO SN020101: URATIBU WA MIPANGO, SERA NA UTAFITI**

21. **Mheshimiwa Spika**; Progamu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti, inasimamiwa na Idara ya Mipango Sera na Utafiti na ina jukumu la kuratibu na kusimamia utayarishaji na utekelezaji wa Sera, Sheria, Bajeti, Miradi na Mipango ya Taasisi zote zilizomo ndani ya Wizara. Pia, Programu inaratibu ufanyaji wa tafiti, ufuatiliaji na kuimarisha mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Vile vile, Programu hii ilipewa jukumu la kuratibu shughuli za Kamati ya Usimamizi na Udhibiti wa Ujenzi (DCU). Hadi kufikia Machi, 2024, Programu hii imefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Imeratibu utayarishaji wa Sera ya Maendeleo ya Miji na Sera ya Maendeleo ya Makaazi, ambapo rasimu za awali za Sera hizo zimekamilika pamoja na Mpango

wa utekelezaji na Mkakati wa Mawasiliano wa Sera ambao unaainisha namna Wadau watakavyoelimishwa vipengele na mikakati ya Sera. Sera hizo zimepitiwa na Wadau kwa kutoa maoni ya kuimarisha rasimu za Sera ikiwemo Masheha, Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi. Sera hizo zipo katika hatua ya kupelekwa katika vyombo vya kutoa maamuzi.

ii. Imekamilisha mapitio ya Sheria ya Mthamini Mkuu wa Serikali na kuandaa Mswada wa Sheria ya Ofisi ya Mthamini Mkuu ambayo inaanzisha Bodi ya Usajili, inasimamia na kudhibiti taaluma ya kazi za uthamini na mambo yanayohusiana nayo. Pia, imefanya mapitio ya Sheria ya Mahakama ya Ardhi na kuandaa Mswada wa Sheria ya Baraza la Ardhi na kudhibiti Kodi za Nyumba. Sheria zote hizo zimeanza kuwasilishwa katika vyombo vya maamuzi. Aidha, Wizara imekamilisha uandaaji wa Kanuni ya Tozo za Ardhi.

iii. Inaendelea kufanya marekebisho ya Sheria na Kanuni mbali mbali za Wizara ili ziendane na mabadiliko ya kiutendaji ya Wizara. Jumla ya Sheria tano (5) na Kanuni nne (4) zinaendelea kufanyiwa mapitio ikiwemo Sheria ya Utambuzi namba 8/1990, Sheria ya Kamisheni ya Ardhi namba 6/2015, Sheria ya Umiliki wa Ardhi namba 12/1992, Sheria ya Upimaji namba 9/1990 na 'Decree' ya Mipango Miji namba 85/1955. Vile vile, hatua za uandaaji wa Kanuni ya Utambuzi, Kanuni ya Miundombinu ya Taarifa za Mfumo ya Ardhi, Kanuni za Uhaulishaji wa Ardhi na Kanuni za Ugawaji wa Viwanja zinaendelea.

iv. Kuendelea na hatua za Maandalizi ya ujenzi wa Mfumo wa Usimamizi na Usajili wa Taarifa za Ardhi (Land Administration and Registration Information System (LARIS) ambao una lengo la kuimarisha shughuli za usimamizi wa ardhi ikiwemo upimaji, mipango miji, usajili, utambuzi na uthamini.

v. Imeandaa Mpango Mkakati wa Wizara wa Miaka mitatu 2023 hadi 2026 ambao utakua ni Muongozo wa Wizara katika kutekeleza majukumu yake. Mpango Mkakati umezingatia utekelezaji wa Mipango ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ikiwemo Dira 2050, Mpango wa Taifa wa Maendeleo Zanzibar 2021-2026, Ilani ya CCM 2020-2025, Malengo Endelevu ya Dunia 2030 na Ajenda ya Afrika 2063.

vi. Imefanya ufuatiliaji wa shughuli za Wizara ikiwemo Miradi ya ujenzi wa nyumba za Makaazi Mombasa (Kwa Mchina) ambapo kazi ya ujenzi inaendelea kwa kasi sana ambapo hadi Machi, 2024 ujenzi huu umefikia asilimia 69 na Ujenzi na ukarabati wa Nyumba za Shirika Darajani ambao umefikia asilimia 58. Pia, imetembelea maeneo yaliyopendekezwa kujengwa nyumba za gharama nafuu na biashara Unguja na Pemba. Maeneo hayo ni pamoja na Chokaani na Chokocho kwa Wilaya ya Mkoani; Pujini na Gomish kwa Wilaya ya Chake Chake; Chumbuni - Wilaya ya Mjini; Ubago na Dunga – Wilaya ya Kati na Pangeni Wilaya ya Kaskazini B Unguja.

vii. Ilifanya ziara ya mashirikiano ya kujifunza katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makaazi ya

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) katika Sekta ya Ardhi na Makaazi. Katika ziara hiyo Watendaji na Viongozi walijifunza namna Wizara hiyo inavyotekeleza majukumu yake katika maeneo tofauti ikiwemo matumizi ya mifumo ya kielektroniki, utatuzi wa changamoto zinazohusiana na ardhi na kutembelea Miradi ya Nyumba inayosimamiwa na Shirika la Nyumba la Taifa.

viii. Iliandaa kikao kilichowashirikisha Wataalamu kutoka Chuo cha Ardhi - Dar-es-Salam kilichokuwa na lengo la kutoa maoni ya kuboresha Mfumo wa Usimamizi na Usajili wa Taarifa za Ardhi (LARIS) Zanzibar. Pia, ilishiriki Vikao vya maandalizi ya Maadhimisho ya Miaka 60 ya uhusiano wa Kidiplomasia kati ya Tanzania na China katika kuimarisha Sekta Milki ambapo Maadhimisho hayo yanatarajiwa kufanyika mwaka huu kwa kufanya Makongamano na shughuli mbali mbali.

ix. Imeandaa andiko la nadharia la kufanya utafiti wa kuangalia uimara wa huduma zinazotolewa na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi ili kuweza kuona mafanikio pamoja na kubaini changamoto zilizopo katika kuimarisha huduma zinazotolewa na Wizara.

x. Imeshiriki katika kikao cha uchambuzi wa taarifa za matokeo ya Sensa ya Majengo ya mwaka 2022. Vikao hivyo vililenga kukamilisha uandaaji wa taarifa za Majengo kwa ngazi ya Mikoa na Halmashauri kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili.

xi. Imechambua na kupitisha maombi ya vibali vya ujenzi vilivyowasilishwa ambapo jumla ya vibali 392

vimetolewa. Kati ya hivyo, vibali 187 vya ujenzi wa majengo mapya, 162 ujenzi wa majengo yanayoendelea na 43 Miradi ya Maendeleo kupitia ZIPA.

xii. Imefanya ukaguzi wa kawaida kwa maeneo ya ujenzi kwa lengo la kuangalia iwapo wananchi wanajenga kwa kufuata taratibu na Sheria zilizowekwa kulingana na vibali walivyoombea. **Kiambatanisho nambari 2** kinafafanua.

xiii. Imechukua hatua kwa wanaojenga bila ya kukata vibali au kwenda kinyume na vibali walivyopewa wakati wa ujenzi wao ikiwemo kuvunja Nyumba Mbili (02) kwa wananchi waliovamia katika eneo la Serikali, Misingi Mitatu (03) ya nyumba, kuta Tatu (03) za uzio, maduka Matatu (03) yaliyojengwa katika hifadhi za barabara, kuta Tano (05) kwa wananchi walioziba njia na maeneo Manne (04) ya wananchi waliojenga katika njia za maji. Aidha, notisi Mia Mbili na Sitini na Mbili (262) za kusitisha ujenzi zimetolewa kwa sababu ya kutofuata taratibu za ujenzi.

22. **Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2023/24, Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti ilipangiwa kukusanya jumla ya **TZS 1,476,000,000** kutokana na Ada za Vibali vya Ujenzi. Aidha, kwa kipindi cha Miezi Tisa Programu ilipangiwa kukusanya jumla ya **TZS 1,104,500,000** ambapo hadi kufikia Machi 2024, fedha zilizokusanywa ni **TZS 449,676,401** ambayo sawa na **asilimia 41** ya makadirio ya fedha kwa Miezi Tisa na **asilimia 30** ya makadirio ya Mwaka.

23. **Mheshimiwa Spika**; Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, jumla ya **TZS 744,430,000** (**TZS 187,412,000** Mishahara na **557,018,000** Matumizi ya Kawaida) ziliidhinishwa kutumika kwa utekelezaji wa Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti. Kwa kipindi cha Miezi Tisa Programu hii ilikadiriwa kutumia jumla ya **TZS 587,721,787** (**TZS 140,559,087** Mishahara na **TZS 447,162,700** Matumizi ya kawaida). Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **TZS 291,326,835** ( **TZS 162,796,840** Mishahara na **TZS 128,529,995** Matumizi ya kawaida) zilipatikana sawa na **asilimia 50** kwa Miezi Tisa na **asilimia 39** ya makadirio kwa mwaka.

24. **Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti itaendelea kuandaa na kuzifanyia mapitio Sera za Wizara ambapo Sera mbili zitaandaliwa (Sera ya Maendeleo ya Miji na Sera ya Maendeleo ya Makaazi) na Sera moja itafanyiwa mapitio (Sera ya Ardhi). Aidha, Sheria nne zitaendelea kufanyiwa mapitio; Kanuni 10 za utekelezaji wa Sheria za Wizara zitaandaliwa na kufanya tafiti mbili (Tathmini ya ufanisi wa huduma zinazotolewa na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi na Tathmini ya zoezi la uhaulishaji wa ardhi na migogoro ya Ardhi). Pia, itaendelea kukusanya takwimu za Sekta ya Ardhi, Makaazi na Nyumba; itafanya ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za Miradi na Programu za Wizara; itasimamia shughuli za DCU na kuimarisha mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa katika Sekta ya Ardhi, Nyumba na Makaazi.

25. **Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Programu hii imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS 2,127,000,000** kutokana na mapato yatokanayo na utoaji wa Vibali vya ujenzi.

26. **Mheshimiwa Spika**; Ili kuiwezesha Programu hii kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS 5,836,498,000** ambapo **TZS 236,498,000** Mishahara, **TZS 600,000,000** Matumizi ya kawaida na **TZS 5,000,000,000** kwa kazi za Maendeleo.

**PROGRAMU NDOGO SN020102: UTAWALA NA UENDESHAJI**

27. **Mheshimiwa Spika**; Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji inayosimamiwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi yenye jukumu la kusimamia uendeshaji wa shughuli za Wizara, usimamizi wa rasilimali watu kwa kuandaa Mipango ya kuwajengea uwezo Watumishi, kuimarisha mazingira bora ya kazi, kushughulikia haki na stahiki za Watumishi, kuhakikisha kuwepo kwa Watendaji wa kutosha na wenye sifa ndani ya Wizara na Taasisi pamoja na kusimamia nidhamu kwa watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake. Hadi kufikia Machi, 2024, imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Imelipa likizo na stahiki kwa Wafanyakazi Hamsini na Saba (57) ambapo wafanyakazi Kumi na Nne(14) wamepatiwa posho la likizo, Tisa (9) Posho za muda wa ziada na watatu (3) Ubani wa Kufiwa. Aidha,

wafanyakazi 31 wamefanyiwa tathmini ya upimaji utendaji kazi. **Kiambatanisho nambari 3** Kinafafanua.

ii. Imeratibu nafasi za ajira Sita (6) ambapo nafasi Tatu (3) zimeajiriwa katika fani ya Mipango miji (1), Afisa Kumbukumbu Mmoja (1) na Mhandisi Ujenzi Mmoja (1). Aidha, usaili umekamilika kwa nafasi Tatu (3), Afisa Tehama Mmoja(1), Afisa Sheria Mmoja (1) na Afisa Mipango Miji Mmoja (1), kwa sasa Wizara inasubiri hatua za uajiri zikamilike. Aidha, Wizara imepata kibali chengine cha uajiri kwa nafasi ya Afisa Manunuzi Mmoja (1) na Afisa Mipango Miji Mmoja (1), hatua za utekelezaji wake zinaendelea.

iii. Imewapatia wafanyakazi Thalathini na Nne (34) Mafunzo ya muda mrefu na Wafanyakazi Mia Moja Hamsini na Sita (156) mafunzo ya muda mfupi kwa lengo la kuwaongezea ujuzi wa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. **Kiambatanisho nambari 4 (a)** na **(b)** kinafafanua.

iv. Imetengeneza Habari Mia Nne na Kumi na Tisa (419) na kuzirusha katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii. Aidha, Makala Kumi na Nane (18) zimeandaliwa, Matangazo Manane (8) yamerushwa hewani, vipindi Tisa (9) vya moja kwa moja kupitia televisheni kwa lengo la kuelimisha jamii juu ya utekelezaji wa shughuli za Wizara.

v. Imesimamia upatikanaji wa huduma za kiofisi kwa asilimia 100% ikiwemo malipo ya umeme, vifaa vya kuandikia, huduma za ulinzi na usafi, matengenezo ya Viyoyozi na upatikanaji wa maji safi na salama kwa lengo la kuhakikisha shughuli za Wizara zinatekelezeka kwa Ubora na Ufanisi.

vi. Imesimamia masuala ya usafiri kwa kazi za Ofisi kwa kufanya matengenezo ya kawaida kwa gari Tatu (3) na kuvifanyia "services" vyombo Kumi na Tatu (13) pamoja na ununuzi wa mafuta kwa ajili ya matumizi ya Wizara.

vii. Imefanya Usambazaji wa Waya za "network" kutoka "ghorofa ya chini" hadi ghorofa namba tatu. Pia, imefanya manunuzi ya leseni ya kifaa cha huduma ya mtandao (SOPHOS) ambayo inawezesha kuipa ulinzi Mifumo ya Network ya Wizara. Aidha, imefanya ununuzi wa UPS Moja (1) ambayo iliharibika ndani ya "Server Room".

viii. Imesuluhisha migogoro ya ardhi 102 na kupatiwa ufumbuzi wake kupitia Kamati ya Usuluhishi wa Migogoro pamoja na kufuatilia maeneo yenye migogoro hiyo ikiwemo Jambiani, Tunguu, Kijitoupele, Chwaka, Kidoti, Mahonda, Kama, Mwakaje, Nyerere, Mbweni, Kianga, Pongwe Pwani, Pwani Mchangani na Kendwa kwa Unguja na Kinyasini, Msaani na Gombani kwa Pemba.

ix. Imezifanyia kazi jumla ya Ripoti Tatu (3) za hoja za mkaguzi wa ndani.

28. **Mheshimiwa Spika;** Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Programu hii iliidhinishiwa kutumia jumla ya **TZS 3,149,062,000** (**TZS 2,744,061,000** Mshahara na **TZS 405,001,000** Matumizi ya kawaida). Kwa kipindi cha Miezi Tisa Programu hii imekadiriwa kutumia jumla ya **TZS 2,369,592,550** (**TZS 2,058,045,750** Mishahara na **TZS 311,546,800** Matumizi ya kawaida). Hadi kufikia Machi, 2024, fedha zilizopatikana ni **TZS 1,562,016,994** (**TZS 1,366,245,631** Mishahara na **TZS 195,771,363** Matumizi ya kawaida) sawa na **asilimia 66** ya makadirio kwa Miezi Tisa na **asilimia 50** kwa mwaka.

29. **Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu ndogo ya Uendeshaji na Utumishi itaratibu shughuli za uendeshaji na usimamizi wa rasilimali za Wizara; itawajengea uwezo wafanyakazi (80) kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu (10) na muda mfupi (70) na kuwapatia stahiki zao kwa mujibu wa taratibu za Utumishi; itaendelea kuratibu upatikanaji wa ajira (10) ili kupata watendaji wa kutosha na wenye sifa; itafanya mapitio ya Mkataba wa huduma kwa wateja na itaratibu mapitio ya miundo na majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Wizara ili kuleta ufanisi zaidi katika utekelezaji wa kazi na kuimarisha ushirikiano baina ya Wizara.

30. **Mheshimiwa Spika**; Ili kuiwezesha Programu hii kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS 1,821,535,000** kati

ya hizo **TZS 1,416,535,000** Mishahara na **TZS 405,000,000** kazi za kawaida.

## PROGRAMU NDOGO SN020103: URATIBU WA SHUGHULI ZA WIZARA PEMBA

31. **Mheshimiwa Spika**; Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba inatekelezwa na Afisi Kuu Pemba ambayo ina jukumu la kuratibu na kusimamia Utawala na Mipango ya kazi zote za Wizara kwa upande wa Pemba ikiwemo Programu na Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2024 Programu hii imetekeleza kazi zifuatazo: -

    i. Imewapatia mafunzo Wafanyakazi Ishirini na Tisa (29), kati ya hao watano (5) mafunzo ya muda mrefu, Ishirini na Mbili (22) mafunzo ya muda mfupi na Wawili (02) mafunzo ya ndani. Aidha, imelipa Wafayakazi 46 Stahiki zao ikiwemo safari za kikazi 27, likizo wafanyakazi 2, ubani Wafanyakazi watano (5), Motisha ya Mfanyakazi bora Mmoja (01) na Wafanyakazi 11 malipo ya muda wa ziada. Pia, Wizara imefanya ununuzi wa vifaa vya kuendeshea Ofisi ikiwemo vifaa vya kuandikia pamoja na upatikanaji wa huduma za umeme, maji, usafi na ulinzi. Vile vile, imefanya ununuzi mafuta kwa ajili ya ufuatiliaji wa shughuli za Ofisi.

    ii. Imeandaa ‘documentary’ ya Mafanikio ya Wizara kwa kipindi cha miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na mafanikio ya miaka mitatu ya utekelezaji wa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi.

iii. Imefanya ufuatiliaji wa kazi za Ofisi na Miradi ya Maendeleo kama ifuatavyo:-

a. Mradi wa ujenzi wa Jengo la Biashara na Makaazi lililopo Mabatini Chake Chake Pemba ambapo hatua iliyofikiwa ni Umalizaji wa plasta katika sehemu za maduka pamoja na 'fitting' ya umeme katika ghorofa ya kwanza na umwagaji zege katika ghorofa ya pili.

b. Maeneo yanayotarajiwa kujengwa ujenzi wa Mradi mkubwa unaojulikana kwa jina la Nyumba za bei nafuu ambapo jumla ya nyumba 400 zinatarajiwa kujengwa katika Wilaya zote za Pemba Mbuyuni, Mkanyageni, Pujini, Tibirinzi, Kinyasini, Kinyikani, Tumbe Magharibi na Sizini.

c. Maeneo yaliyopangwa kuwa Miji mipya (Mfikiwa na Mvumoni -Furaha).

d. Ufuatiliaji wa maeneo 9 ya migogoro ya Ardhi na nyumba kati ya migogoro 11 iliyopokelewa na iliyotolewa maamuzi 7.

32. **Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu hii ilipangiwa kukusanya jumla ya **TZS 28,000,000** kutokana na vyanzo vyake vya mapato kwa mwaka na ilipangiwa kukusanya **TZS 20,060,000** kwa kipindi cha Miezi Tisa. Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **TZS 12,289,400** zimekusanywa sawa na **asilimia 61** ya makadirio ya Miezi Tisa na **asilimia 44** ya mwaka.

33. **Mheshimiwa Spika**; Programu ndogo ya Uratibu wa shughuli za Wizara Pemba ilipangiwa kutumia jumla ya

**TZS 1,054,004,000** (**TZS 805,423,000** Mishahara na **TZS 248,581,000** Matumizi ya Kawaida). Kwa kipindi cha Miezi Tisa, Programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS 819,353,640** (**TZS 215,285,700** Mishahara na **TZS 604,067,940** Matumizi ya kawaida). Hadi kufikia Machi, 2024, fedha zilizotumika ni jumla ya **TZS 615,302,101** (**TZS 527,662,101** Mishahara na **TZS 87,640,000** Matumizi ya Kawaida) sawa na **asilimia 75** ya fedha zilizopangwa kwa Miezi Tisa na **asilimia 58** kwa Mwaka.

34. **Mheshimiwa Spika**; Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu ya Uratibu wa shughuli za Wizara Pemba itaendelea kuratibu shughuli za Wizara Pemba; itaimarisha kazi na usimamizi wa Mipango, Bajeti, na Ufuatiliaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa upande wa Pemba, itaimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi kwa Wafanyakazi, itawapatia mafunzo ya muda mfupi Wafanyakazi Watatu (3), mafunzo ya muda mrefu Wafanyakazi Watatu (3) na itasimamia ajira mpya kwa Wafanyakazi Tisa (9).

35. **Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu hii imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS 43,000,000** kutokana na vyanzo vyake vya mapato.

36. **Mheshimiwa Spika**; Ili kuiwezesha Programu hii kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS 864,936,000** ambapo **TZS 419,836,000** Mishahara na **TZS 445,100,000** kazi za kawaida.

37. **Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu Kuu PN0201 ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara

ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS 2,170,000,000** kutokana na vyanzo vyake vya mapato.

38. **Mheshimiwa Spika**; Ili kuiwezesha Programu Kuu PN0201 ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS 8,522,969,000** ambapo **TZS 2,072,869,000** Mishahara, **TZS 1,450,100,000** kazi za Kawaida na **TZS 5,000,000,000** Miradi ya Maendeleo.

**PROGRAMU KUU PN0202: USIMAMIZI WA ARDHI**

39. **Mheshimiwa Spika**; Programu Kuu PN0202 ya Usimamizi wa Ardhi ina jukumu la kuhakikisha usalama na umiliki wa matumizi ya ardhi (Security of Land Tenure) kwa Wananchi na ina Programu ndogo moja. Kwa mwaka wa Fedha 2023/2024, ilikadiriwa kukusanya **TZS 280,000,000** na **TZS 209,250,000** kwa kipindi cha Miezi Tisa. Hadi kufikia Machi, 2024, **TZS 111,005,145** zilikusanywa sawa na **asilimia 53** kwa Miezi Tisa na **asilimia 40** kwa mwaka.

40. **Mheshimiwa Spika**; Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Programu Kuu PN0202 ya Usimamizi wa Ardhi iliidhinishiwa kutumia jumla ya **TZS 801,284,000** (**TZS 342,604,000** Mishahara, **TZS 213,680,000** Ruzuku na **TZS 245,000,000** kwa Matumizi ya kawaida) na **TZS 605,458,540** (**TZS 256,953,540** Mishahara, **TZS 183,750,000** Matumizi ya kawaida na **TZS 164,755,000** Ruzuku) kwa kipindi cha Miezi Tisa. Hadi kufikia Machi, 2024, fedha zilizopatikana

ni **TZS 419,433,689** ( **TZS 268,712,047** Mishahara, **TZS 73,698,642** Matumizi ya kawaida na **TZS 77,023,000** Ruzuku) sawa na **asilimia 68** kwa Miezi Tisa na **asilimia 52** kwa mwaka.

**PROGRAMU NDOGO SN020201: USIMAMIZI WA ARDHI**

41. **Mheshimiwa Spika**; Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi inatekelezwa na Taasisi Tatu (3) za Wizara. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi ilitekeleza shughuli zote zinazohusiana na masuala ya Ardhi kupitia Taasisi zake kama ifuatavyo: -

**HN02020108: UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI – MAHAKAMA YA ARDHI**

42. **Mheshimiwa Spika**; Huduma hii inatekelezwa kupitia Mahakama ya Ardhi ambayo imeanzishwa chini ya Sheria Namba 7 ya Mwaka 1994. Lengo la kuanzishwa kwake ni kupokea, kusikiliza na kuyatolea uamuzi mashauri yanayotokana na migogoro ya ardhi yanayowasilishwa na wananchi.

43. **Mheshimiwa Spika**; Hadi kufikia Machi, 2024, Mahakama ya Ardhi imetekeleza kazi zifuatazo:

   i. Imepokea kesi mpya Mia Moja na Thalathini na Tano (135) ambazo zimefunguliwa Unguja na Pemba. Mahakama imeendelea kusikiliza kesi hizo pamoja na za awali ambapo kesi Mia Moja na Nane (108) zimetolewa uamuzi, sawa na **asilimia 48** ya lengo la kuamua kesi 223

kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2024. **Kiambatanisho nambari 5** kinafafanua.

ii. Imeendelea kutoa elimu katika Mikoa Minne (4) ya Zanzibar kuhusiana na utatuzi wa migogoro ya ardhi, masuala ya utambuzi wa ardhi na taratibu za utekelezaji wa hukumu katika Mahakama. Maeneo yaliyofikiwa ni pamoja na Kiboje - Kusini Unguja, Matemwe na Donge - Kaskazini Unguja, Kiwani - Kusini Pemba na Kiapaka Mtambwe - Kaskazini Pemba. Pia, imetoa elimu kwa jamii kuzitambulisha Mahakama za Ardhi, umiliki ardhi kwa mujibu wa Sheria na utatuzi wa migogoro ya Ardhi kwa njia ya usuluhishi kupitia Maonesho na vyombo vya habari.

44. **Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Mahakama ya Ardhi ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 10,000,000** na T**ZS 7,450,000** ilikadiriwa kukusanya kwa Miezi Tisa. Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **TZS 6,133,821** zilikusanywa sawa na **asilimia 82** ya makadirio kwa Miezi Tisa na **asilimia 61** kwa mwaka.

45. **Mheshimiwa Spika**; Kwa upande wa Matumizi Mahakama ya Ardhi ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS 587,604,000** (**TZS 342,604,000** Mishahara na **TZS 245,000,000** kwa matumizi ya kawaida) na **TZS 440,703,540** (**TZS 256,953,540** Mishahara na **TZS 183,750,000** matumizi ya kawaida) kwa kipindi cha Miezi Tisa. Hadi kufikia Machi, 2024, fedha zilizopatikana ni **TZS 342,410,689** (**TZS 268,712,047** Mishahara na **TZS 73,698,642** Matumizi ya kawaida) sawa na **asilimia 75** ya makadirio kwa Miezi Tisa na **asilimia 58** kwa mwaka.

46. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Mahakama ya Ardhi kupitia Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi itaendelea kupokea, kusikiliza na kutoa maamuzi ya mashauri yanayohusiana na migogoro ya ardhi iliyowasilishwa Mahakamani; itayatolea uamuzi mashauri 290 (Unguja 190 na Pemba 100); itaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu migogoro ya ardhi. Pia, itajenga mazingira bora ya kazi kwa kufanya ukarabati wa Mahakama ya Ardhi ya Mwanakwerekwe.

47. **Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Mahakama ya Ardhi imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS 10,000,000** kutokana na Ada ya Mahakama.

48. **Mheshimiwa Spika**; Ili kuiwezesha Mahakama ya Ardhi kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako kuidhinisha **TZS 743,799,000** ambapo **TZS 363,699,000** Mishahara na **TZS 380,100,000** Matumizi ya kawaida.

**HN02020107: KUSIMAMIA NA KUIDHINISHA RIPOTI ZA UTHAMINI – OFISI YA MTHAMINI MKUU WA SERIKALI**

49. **Mheshimiwa Spika**; Huduma hii chini ya Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi inatekelezwa na Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali ambayo imeanzishwa kwa Sheria Namba 5 ya Mwaka 2015 kwa madhumuni ya kuhakikisha usimamizi mzuri wa uthaminishaji mali kwa malengo mbalimbali ya Sekta ya Umma, Biashara na Wananchi kwa ujumla. Kazi kuu ya Mthamini Mkuu wa Serikali ni kuthibitisha kazi za

uthamini zinazofanywa nchini na Wathamini wa Taasisi za Serikali na Taasisi binafsi.

50. **Mheshimiwa Spika**; Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali imetekeleza kazi zifuatazo:

i. Imethibitisha ripoti 365, kati ya hizo 17 ni ripoti za uthamini mali kwa ajili mikopo (Mortgage purpose), 130 ripoti za uthamini mali kwa ajili ya thamani (Market Value Determination), 120 ripoti za uthamini mali kwa ajili ya mirathi (Inheritance purpose), 96 ripoti ya uthamini mali kwa ajili ya fidia (Compensation purpose) na 2 ni ripoti za uthamini kwa ajili ya uhaulishaji.

ii. Imefanya uthamini katika Miradi ya kimkakati inayotekelezwa na Serikali nchini ikiwemo Mradi wa Bandari Jumuishi Mangapwani, Upanuzi wa Barabara za Mjini Unguja na Pemba, Miradi ya Umeme na Maji, Miradi ya Masoko na Maeneo ya Uwekezaji pamoja na Miradi ya Skuli na Hospitali za Wilaya.

iii. Imeandaa Miongozo ya Uthamini ambayo itasaidia kupunguza changamoto katika masuala ya Uthamini hasa wa fidia. Miongozo hiyo inajumuisha Rasimu ya Muongozo wa Uthamini wa Fidia; Rasimu ya Muongozo wa Masafa ya Miti na Mazao (Trees and Crops spacing); Rasimu ya viwango vya Thamani za Ujenzi na Rasimu ya Muongozo wa Haki ya Matumizi ya Ardhi (Land Rates).

iv. Imetoa elimu ya Uthamini kwa wadau kupitia mikutano na vyombo vya habari kwa ajili ya kutoa uelewa kwa jamii kuhusu umuhimu wa uthaminishaji mali kwa

malengo tofauti hasa katika uthamini wa fidia ambapo wananchi wengi wanaathirika na Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa na Serikali, uthamini kwa mikopo Benki, uthamini kwa ajili ya uhaulishaji ardhi, uthamini kwa ajili ya Bima, uthamini kwa ajili ya mirathi n.k.

v. Inaendelea na taratibu za kufungua Ofisi ya Mthamini kwa upande wa Pemba kwa lengo la kuongeza ufanisi na upatikanaji wa huduma za uthamini kwa haraka ambapo hatua za kupatikana wafanyakazi na vitendea kazi zinaendelea.

vi. Inaendelea kusajili Wathamini na kuwapatia leseni ambapo maombi ya wathamini 16 na Kampuni 4 za uthamini yamepokelewa na kufanyiwa kazi.

51. **Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu hii kupitia Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 270,000,000** na **TZS 201,800,000** ilikadiriwa kukusanya kwa kipindi cha Miezi Tisa. Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya **TZS 104,871,324** zilikusanywa sawa na **asilimia 51** ya makadirio kwa Miezi Tisa na **asilimia 39** ya makadirio ya mwaka.

52. **Mheshimiwa Spika**; Kwa upande wa Matumizi Ofisi ilipangiwa kutumia Ruzuku jumla ya **TZS 213,680,000** kwa mwaka na **TZS 164,755,000** kwa kipindi cha Miezi Tisa. Hadi kufikia Machi, 2024, fedha zilizopatikana ni **TZS 77,023,000** sawa na **asilimia 47** ya makadirio ya Fedha zilizopangwa kwa Miezi Tisa na **asilimia 36** kwa mwaka.

53. **Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali kupitia Programu

ndogo ya Usimamizi wa Ardhi itahakiki na kuidhinisha ripoti 580 za uthamini wa rasilimali; itaendelea kusajili na kuwapatia leseni Wathamini 50; itatoa elimu ya Uthamini kwa Wadau; itakamilisha utayarishaji wa Miongozo ya Uthamini ikiwemo Muongozo Mkuu wa Fidia Zanzibar; itaweka kumbukumbu za mali zilizofanyiwa Uthamini katika Mfumo na itaandaa Kanuni za Sheria ya Usajili wa Wathamini.

54. **Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS 500,000,000** kutokana na vyanzo vyake vya mapato.

55. **Mheshimiwa Spika;** Ili Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi chini ya Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa Fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako kuidhinisha Ruzuku ya jumla ya **TZS 256,400,000** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida.

**HN02020101: UPANGAJI NA USIMAMIZI WA ARDHI – KAMISHENI YA ARDHI**

56. **Mheshimiwa Spika**; Huduma hii ya Progaramu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi inatekelezwa na Kamisheni ya Ardhi ambayo imeanzishwa kwa Sheria Namba 6 ya Mwaka 2015 kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria za Sekta ya Ardhi na kuziunganisha Idara zote zinazosimamia matumizi na maendeleo ya ardhi. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamisheni ya Ardhi imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Imetayarisha na imetoa hati 880 (614 Unguja na 266 Pemba) za haki ya matumizi ya Ardhi. Pia, imehakiki Hati

za haki ya matumizi ya Ardhi 367 (247 Unguja na 120 Pemba). Imetayarisha na kutoa Mikataba ya Ukodishaji wa Ardhi kwa Wawekezaji 278 (257 Unguja na 21 Pemba). Aidha, imefanya na kutoa kazi za uthamini 301 (177 Unguja na 124 Pemba) na imetoa hati za utambuzi 947 (556 Unguja na 391 Pemba).

ii. Imekagua maeneo 478 ya uhaulishaji pamoja na kufanya Ziara katika maeneo Saba (7) yaliogundulika na changamoto katika uhaulishaji. Aidha, imepokea na kuyafanyia kazi maombi ya uhaulishaji 1,192, ambapo 966 yamekubaliwa, 92 yameelekezwa na 134 yamekataliwa.

iii. Imepima viwanja 1,411 (843 Unguja na 568 Pemba) katika maeneo ya makaazi, taasisi, mashamba, eka na vitega uchumi pamoja na kupima vianzio vya upimaji 25 (15 Unguja na 10 Pemba). Aidha, imetayarisha ramani 2,351 (1,614 Unguja na 737 Pemba) na imekusanya taarifa 6 za vipimo vya kupwa na kujaa kwa Maji ya Bahari. Vile vile, imefanikiwa kutayarisha ZUPIN 1,088 (632 Unguja na 456 Pemba) na imetoa taarifa za utunzaji na upatikanaji wa taarifa za Ardhi 1,469 (998 Unguja na 471 Pemba).

iv. Inaendelea na zoezi la kuimarisha Miji minne (4) kwa kuweka mipango na ramani ambayo ni Kibuteni, Paje - Jambiani na Muembeshauri kwa Unguja na Furaha kwa Pemba. Aidha, inaendelea na uimarishaji wa Mipango ya Maendeleo kwa Vijiji ambavyo vipo karibu na maeneo ya uwekezaji (EPZ) Fumba, Nyamanzi na Bweleo kwa Unguja na Makangale (Mji wa Utalii) kwa Pemba.

v. Imetoa miongozo ya matumizi ya ardhi (Land use permit) 1,555 (Unguja 1,370 na Pemba 185).

vi. Imesajili viwanja 552 (431 Unguja na Pemba 121) na imetengeneza kadi 1,194 (844 Unguja na 350 Pemba). Pia, imehakiki maeneo 504 (357 Unguja na 147 Pemba). Aidha, hati 468 (398 Unguja na 70 Pemba) zimelipiwa ada ya usajili na maeneo 16 (14 Unguja na 2 Pemba) yameendelezwa kiusajili.

vii. Imetoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa Uhaulishaji, Matumizi bora ya Ardhi, usajili wa Ardhi na Sheria za Kamisheni ya Ardhi. Jumla ya vipindi 12 vimerushwa hewani na mikutano 31 (24 Unguja na 7 Pemba) imefanyika.

viii. Imewapatia mafunzo ya muda mfupi Wafanyakazi 33 na mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi (15). Pamoja na kufanya mafunzo ya ndani kwa watumishi. Aidha, iliwapatia mafunzo ya awali ya kuingia kazini (induction course) wafanyakazi (10) kwa lengo la kuthibitishwa kazi.

ix. Imeratibu upatikanaji wa wafanyakazi wapya 7 (4 Unguja Afisa Mipango miji na vijiji, Afisa Upimaji, Afisa Uchoraji na 3 Pemba Afisa Mipango miji, na Afisa Tehama na Msaidizi Afisa Sheria)

x. Imeimarisha mazingira bora ya kazi kwa kulipia huduma ya maji na umeme. Pia imefanya ununuzi wa samani, kompyta tatu (3) na vifaa vya kuandikia (stationaries) pamoja na kusimamia vyombo vya usafiri kwa kuvifanyia matengenezo madogo madogo.

xi. Wafanyakazi 69 wamelipwa stahiki zao ikiwemo 41 posho za likizo, 26 malipo baada ya saa za kazi na 2 ubani wa ufiwa.

xii. Imefanya vikao vitatu (3) vya Bodi ya Kamisheni ya Ardhi pamoja na kufanya ziara ya kutembelea majengo na maeneo ya Kamisheni ya Ardhi kwa Unguja na Pemba na kupatiwa Mafunzo juu ya Sheria za Kamisheni.

xiii. Imeshiriki katika uandaaji wa Sera ya Maendeleo ya Miji na Sera ya Maendeleo ya Makaazi pamoja na uandaaji wa Mpango wa utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Miji na vikao vya maandalizi ya Bajeti.

xiv. Imefanya Ufuatiliaji na Tathmini katika maeneo ya ujenzi wa Kituo cha Masjala ya Ardhi kilichopo Mwanakwerekwe na Makunduchi kwa lengo la kuangalia utekelezaji wa shughuli zilizopangwa na imefanya mafunzo kwa waandishi wa habari 30 juu ya umuhimu wa Sheria na majukumu ya Kamisheni ya Ardhi.

57. **Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka fedha 2023/2024, Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi kupitia huduma ya Upangaji na Usimamizi wa Ardhi chini ya Kamisheni ya Ardhi ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 2,750,890,000** kutokana na ada ya uthamini, muongozo wa matumizi ya ardhi, nyaraka ya ardhi, upimaji wa ardhi, usajili wa ardhi na uhaulishaji ardhi na kwa kipindi cha Miezi Tisa ilikadiriwa kukusanya **TZS 765,108,230**. Hadi kufikia Machi 2024, ilifanikiwa kukusanya jumla ya **TZS 4,832,582,064** sawa na **asilimia 632** kwa Miezi Tisa na **asilimia 176** ya Mwaka.

58. **Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi chini ya Kamisheni ya Ardhi ilikadiriwa kutumia jumla ya **TZS 9,985,300,000** (**TZS 3,040,724,000** Mishahara, **TZS 1,621,500,040** kazi za kawaida, **TZS 773,075,960** Ruzuku ya Uhaulishaji wa Ardhi pamoja na **TZS 4,550,000,000** kazi za Maendeleo) na **TZS 4,262,606,856** (**TZS 2,280,000,000** Mishahara, **TZS 1,402,795,886** Matumizi ya kawaida, **TZS 579,806,970** Ruzuku na **TZS 4,082,400,000** kwa Miradi ya Maendeleo) kwa kipindi cha Miezi Tisa.

59. **Mheshimiwa Spika**; Hadi kufikia Machi, 2024, fedha zilizopatikana ni **TZS 3,264,514,356** (**TZS 2,225,505,356** Mishahara, **TZS 944,586,000** Matumizi ya kawaida na **TZS 94,423,000** Ruzuku) sawa na **asilimia 77** kwa Miezi Tisa na **asilimia 33** ya fedha zilizopangwa kwa mwaka na hakuna fedha ya kazi za Maendeleo iliyoingizwa.

60. **Mheshimiwa Spika**; Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi kupitia Kamisheni ya Ardhi itaimarisha upatikanaji wa hati za haki ya matumizi ya ardhi 3,300, Mikataba ya ukodishwaji ardhi 600, pamoja na kuandaa na kusimamia mikataba ya ukodishwaji wa ardhi; itaratibu na kufanya Uthamini 2,400; itafanya Utambuzi wa Ardhi katika meneo 10 pamoja na kuvitambua viwanja 1,500.

61. **Mheshimiwa Spika**; Vile vile, Kamisheni imepanga kuendelea kuratibu na kusimamia masuala ya uhaulishaji katika maeneo 2,500; kuyapima na kutayarisha ramani za maeneo 2,250 na kuyapima maeneo 400 ya Serikali. Pia,

itaendeleza zoezi la utayarishaji wa ramani za msingi 14 za baharini (Hydrographical Survey); itaandaa na kusimamia alama msingi 12 za upimaji; itatayarisha nambari 1,400 za ZUPIN na ramani kwa ajili ya hati na uwekaji wa kumbukumbu za upimaji na ramani.

62. **Mheshimiwa Spika**; Kamisheni itaandaa Mpango maalum wa matumizi ya ardhi; mpango wa usimamizi na upangaji wa maeneo ya baharini (Marine Spatial Plan); itabainisha, itahakiki na kuyatangaza maeneo saba (7) ya Ardhi ya akiba (land bank) na kutayarisha mpango wa kina kwa ajili ya Ardhi ya akiba, itaimarisha mipango ya maendeleo kwa vijiji ambavyo vipo karibu na maeneo ya uwekezaji (EPZ); itasajili maeneo 2,100 yaliyokamilisha vigezo; pamoja na Kuimarisha mfumo wa uwekaji wa kumbukumbu za usajili na kutoa elimu kwa jamii kuhusu usimamizi na utawala wa ardhi.

63. **Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu ndogo ya Usimamizi wa Ardhi chini ya Huduma ya Upangaji na Usimamizi wa Ardhi inayotekelezwa na Kamisheni ya Ardhi ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, naliomba Baraza lako kuidhinisha Ruzuku ya Mishahara **TZS 3,003,300,000** na **asilimia 50** ya makusanyo yake kutumika kwa ajili ya matumizi mengineyo.

64. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu Kuu PN0202 ya Usimamizi wa Ardhi imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS 510,000,000** kutokana na vyanzo vyake vya mapato.

65. **Mheshimiwa Spika**; Ili kuiwezesha Programu Kuu PN0202 ya Usimamizi wa Ardhi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS 4,003,499,000** ambapo **TZS 3,003,300,000** Ruzuku ya Mshahara, **TZS 743,799,000** (**TZS 363,699,000** Mshahara, **TZS 380,100,000** kazi za kawaida) na **TZS 256,400,000** Ruzuku ya matumizi mengineyo.

66. **Mheshimiwa Spika**; Vile vile, naliomba Baraza lako kuidhinisha matumizi ya **asilimia 50** ya makusanyo ya mapato ya Kamisheni ya Ardhi kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake za kawaida.

## PROGRAMU KUU PN0203: MAENDELEO YA MAKAAZI

67. **Mheshimiwa Spika**; Programu Kuu PN0203 ya Maendeleo ya Makaazi ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa makaazi bora, salama, jumuishi na endelevu kwa wananchi pamoja na kuweka mazingira rafiki kwa Wawekezaji wa Sekta Binafsi katika huduma ya makaazi.

68. **Mheshimiwa Spika**; Programu hii kwa mwaka wa Fedha 2023/2024, ilikadiriwa kukusanya **TZS 350,000,000** na **TZS 256,000,000** kwa kipindi cha Miezi Tisa. Hadi kufikia Machi, 2024, **TZS 526,191,036** zilikusanywa sawa na **asilimia 206** kwa Miezi Tisa na **asilimia 150** kwa Mwaka.

69. **Mheshimiwa Spika**; Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Programu Kuu PN0203 ya Maendeleo ya Makaazi iliidhinishiwa kutumia Ruzuku ya jumla ya **TZS 262,500,000** na **TZS 216,375,000** kwa kipindi cha Miezi

Tisa. Hadi kufikia Machi, 2024, fedha zilizopatikana ni **TZS 101,750,000** sawa na **asilimia 47** kwa Miezi Tisa na **asilimia 39** kwa mwaka.

70. **Mheshimiwa Spika**; Programu Kuu PN0203 ya Maendeleo ya Makaazi inatekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Makaazi, Shirika la Nyumba Zanzibar na Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba kupitia Huduma ya Usajili wa Majengo na Jumuiya ya Kondominio na Huduma ya Utatuzi wa Migogoro kwa Wapangaji wa Nyumba. Programu hii ina Programu ndogo moja SN020301 ya Maendeleo ya Makaazi.

## PROGRAMU NDOGO SN020301: MAENDELEO YA MAKAAZI

## HUDUMA HN02030102 USAJILI WA MAJENGO NA JUMUIYA YA KONDOMINIO

71. **Mheshimiwa Spika;** Programu Ndogo ya SN020301 kupitia huduma ya Usajili wa Majengo na Jumuiya ya Kondominio inatekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Makaazi ambayo imeanzishwa baada ya kufutwa kwa Bodi ya Kondominio iliyokuwa chini ya Sheria ya Kondominio Namba 10 ya Mwaka 2010. Idara ina jukumu la kusimamia Maendeleo ya Makaazi Nchini, kusajili Majengo ya Kondominio, kuratibu na kuhakikisha upatikanaji wa Makaazi bora na nafuu kwa Wananchi pamoja na kusimamia matumizi ya pamoja kwa majengo yenye sehemu zinazomilikiwa na mtu zaidi ya mmoja. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Programu ndogo ya Maendeleo ya Makaazi kupitia Huduma ya Usajili wa Majengo na Jumuiya ya Kondominio inayotekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Makaazi imefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Imesajili Ramani Tisa (09) katika miradi ya Kondominio ambayo ni Furaha Investment Limited uliopo Bwejuu, Dream Company Limited (Awamu 1&2) uliopo Nungwi, Mwerevu Company Limited uliopo Michamvi, Johari Developers Limited uliopo Kizimkazi, Floton Afrika Company Limited uliopo paje, System Design Solution (Awamu 2) ulipo Mbweni, Zanzibar Villas Limited (Awamu 2&3) uliopo Paje na PGH Company Limited uliopo Jambiani.
ii. Imesajili Majengo manne (04) ya Kondominio ambayo ni Zanzibar Villas Limited (Awamu 1&2) ulipo Paje kwa Unguja na Ng'ombeni na Mapinduzi kwa Pemba
iii. Imesajili Umiliki wa Sehemu/fleti Mia Moja na Tisa (109) katika Nyumba za Maendeleo za Kilimani (18), Michenzani (71), Machomane (2), Ng'ombeni (1) na Mapinduzi (2) na nyumba za miradi mipya ya Mbweni (4) na Paje (11). Pia, imefanya kambi maalumu kwa ajili ya zoezi la usajili katika nyumba 14 za Maendeleo Kikwajuni..
iv. Imefanya ukaguzi wa Miradi Tisa (09) katika maeneo ya Mbweni, Nungwi, Kizimkazi, Paje, Kilimani na Michenzani kwa Unguja na Mapinduzi, Ng'ombeni na Uweleni Mkoani Pemba.
v. Imefanya Kikao cha utoaji wa elimu kwa Wakaazi wa Bloki nambari 2 Michenzani kuhusiana na utaratibu wa kuunda Jumuiya ya Usimamizi wa majengo ya Kondominio.
vi. Imeyatembelea na kuyatambua maeneo Ishirini na moja (21) yaliyotengwa na Wizara kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za bei nafuu ambayo ni Kitogani, Mwera

Pongwe, Dunga, Matemwe Mbuyutende, Matemwe - Mlilile, Pale, Donge Kipange, Mkataleni, Kinduni, Mgambo na Matetema kwa Unguja na Finya, konde, Tumbe, Sizini, Pujini, Gomish – Wesha, Chokaani na Chokocho kwa Pemba.

vii. Imeratibu vikao vinne (4) vinavyohusiana na Sekta Milki vilivyohusisha wadau wa Sekta milki wakiwemo Watendaji Wakuu wa Hoteli, Taasisi za Kifedha na Taasisi zote zinazohusiana na ujenzi wa Nyumba kwa lengo la kuwasikiliza, kupokea changamoto pamoja na kutoa mapendekezo ili kuimarisha Sekta ya Makaazi.

72. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu kupitia Idara ya Maendeleo ya Makaazi ilikadiria kukusanya jumla ya **TZS 350,000,000** na **TZS 256,000,000** ilikadiriwa kukusanya kwa kipindi cha Miezi Tisa. Hadi kufikia Machi, 2024, Idara imeweza kukusanya jumla ya **TZS 526,191,036** sawa na **asilimia 206** kwa Miezi Tisa na **asilimia 150** ya makadirio kwa mwaka.

73. **Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu kupitia Huduma ya Usajili wa Majengo na Jumuiya ya Kondominio inayotekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Makaazi ilipangiwa kutumia Ruzuku ya **TZS 168,000,000** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za Kawaida na **TZS 135,000,000** ilipangiwa kutumia kwa Kipindi cha Miezi Tisa. Hadi kufikia Machi, 2024, fedha zilizopatikana ni **TZS 61,835,00**0 sawa na **asilimia 46** makadirio kwa Miezi Tisa na **asilimia 37** kwa mwaka.

74. **Mheshimiwa Spika**; Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu ndogo ya Maendeleo ya Makaazi kupitia

Huduma ya Usajili wa Majengo na Jumuiya ya Kondominio inayotekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Makaazi itasimamia upatikanaji wa maeneo (20) ya Ujenzi wa Nyumba kwa Wananchi pamoja na kuendeleza Sekta ya Makaazi Nchini; itaendelea kufanya usajili wa miradi mipya Kumi na Tano (15) ya Kondominio, Ramani Kumi Tano (15), Majengo, Sehemu/fleti (550) na Jumuiya Kumi (10) za Kondominio Unguja na Pemba; itaandaa miongozo (10) ya Jumuiya za Kondominio pamoja na Kufanya ukaguzi na uhakiki katika miradi ya Kondominio; itaendelea kutoa elimu kwa jamii na Wadau mbalimbali kuhusu kazi za Idara ya Maendeleo ya Makaazi, dhana nzima ya kondominio pamoja na usimamizi na uendeshaji wa Jumuiya zake kwa kuzingatia uwiano wa Kijinsia, Watu wenye Mahitaji Maalum, Maafa na Mabadiliko ya Tabia Nchi;

75. **Mheshimiwa Spika;** Idara ya Maendeleo na Makaazi itaendelea na uratibu wa upatikanaji wa taarifa za Sensa ya Majengo kwa wadau mbalimbali Nchini; itaboresha mashirikiano katika Sekta ya Makaazi Kitaifa, Kikanda na Kimataifa na itajenga uwezo wa Watendaji (6) wa Idara ya Maendeleo ya Makaazi Unguja na Pemba.

76. **Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu ndogo ya Maendeleo ya Makaazi kupitia Huduma ya Usajili wa Majengo na Jumuiya ya Kondominio inayotekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Makaazi imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS 1,590,000,000** kutokana na Ada ya usajili wa Kondominio.

77. **Mheshimiwa Spika**; Ili Programu ndogo ya Maendeleo ya Makaazi chini ya Idara ya Maendeleo ya Makaazi iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka

wa fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS 40,431,432,000** kazi za kawaida na Kazi za Maendeleo ambapo **TZS 176,532,000** Mishahara, **TZS 254,000,000** kazi za kawaida na **TZS 40,000,000,000** fedha za Miradi ya Maendeleo.

**HN02030105 UTATUZI WA MIGOGORO KWA WAPANGAJI WA NYUMBA – BODI YA KUDHIBITI KODI ZA NYUMBA**

78. **Mheshimiwa Spika**; Programu ya Maendeleo ya Makaazi kupitia Huduma ya Utatuzi wa Migogoro kwa Wapangaji wa Nyumba inayotekelezwa na Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba ambayo imeanzishwa kwa Sheria ya kudhibiti kodi za Nyumba, Sura ya 98 ya Mwaka 1953 (Cap. 98 of 1953) kwa lengo la kusikiliza na kuyatolea uamuzi mashauri yanayotokana na migogoro ya upangishaji wa Nyumba za Serikali na Nyumba binafsi. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba imetekeleza kazi zifuatazo: -

i. Imepokea mashauri mapya 27 (Unguja 25 na Pemba 02), hivyo kufanya Bodi hii kwa sasa kuwa na Mashauri 46 (41 Unguja na 5 Pemba). Pia, imefanikiwa kusikiliza mashauri Thalathini na Sita (36) na imeyatolea maamuzi mashauri ya migogoro ya kodi za nyumba 14.

ii. Imetoa elimu kwa jamii kuhusu utendaji wa kazi za Bodi kupitia vyombo vya habari na mikutano.

79. **Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba ilikadiriwa kutumia Ruzuku ya **TZS 94,500,000** na **TZS 81,375,000** ya

Ruzuku kwa Miezi Tisa. Hadi kufikia Machi, 2024, fedha zilizopatikana ni Ruzuku **TZS 39,915,000** sawa na **asilimia 49** ya fedha zilizopangwa kwa Miezi Tisa na **asilimia 42** kwa mwaka.

80. **Mheshimiwa Spika**; Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu ndogo ya Maendeleo ya Makaazi kupitia Huduma ya utatuzi wa Migogoro ya Nyumba inayotekelezwa na Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba itatoa elimu kwa Taasisi za Serikali na jamii kuhusiana na shughuli na majukumu ya kisheria ya Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba Zanzibar na itaongeza ufanisi katika utoaji wa maamuzi ya kesi zinazohusiana na migogoro ya kodi za nyumba kwa kuzitolea maamuzi mashauri Thalathini na Tano (35) Unguja na Pemba.

81. **Mheshimiwa Spika**; Ili kuiwezesha Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako kuidhinisha Ruzuku ya **TZS 105,000,000** kwa utekelezaji wa kazi za kawaida.

**SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR**

82. **Mheshimiwa Spika**; Shirika la Nyumba Zanzibar ni taasisi inayojitegemea iliyoanzishwa kwa Sheria Namba 6 ya Mwaka 2014. Taasisi hii imepewa Mamlaka ya kusimamia na kuendeleza Sekta ya Nyumba Zanzibar kwa kuchangia katika ukuaji wa uchumi na Maendeleo ya Makaazi kwa wananchi wa Zanzibar ili kwenda sambamba na mahitaji ya nyumba kutokana na ongezeko la watu na mahitaji pamoja na utoaji wa huduma za ujenzi, ushauri na uwekezaji. Kwa

mwaka wa fedha 2023/2024, Programu ndogo ya Maendeleo ya Makaazi kupitia Shirika la Nyumba imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Inaendelea na ujenzi wa majengo manne (4) yenye nyumba 72 za Makaazi Mombasa (Kwa Mchina) kwa hatua ya Upigaji wa plasta na 'cobra' za madirisha na milango pamoja na kuanza 'skimming' nje na ndani, uwekaji wa vigae, fremu na milango kwa bloki A, 'grill' za madirisha kwa nyumba za chini kwa bloki zote, mifumo ya umeme kwa bloki zote (second fixing) bloki zote (A,B,C na D) na makabati ya jikoni kwa Bloki A unaendelea. Aidha, kazi hiyo ya ujenzi imefikia asilimia 69.

ii. Inaendelea na ujenzi wa jengo namba 1293/1294- (kwa fundi Abduli) Darajani la ghorofa tatu (03). Kazi ya ujenzi inafanywa na kusimamiwa na Shirika lenyewe na imefikia asilimia 58.

iii. Inaendelea na ujenzi wa Jengo la ghorofa 4 la biashara na makaazi Mkungu Malofa (Mabatini) ChakeChake Pemba. Ujenzi huo unafanywa na Shirika na kusimamiwa na Wakala wa Majengo Zanzibar na umefikia asilimia 50.

iv. Imeanza kazi ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Shirika la Nyumba Pemba Machomane kwa hatua za awali zikiwemo uvunjaji wa jengo lililopo, uondoshaji wa kifusi na ujenzi wa msingi na uwekaji wa uzio (fencing) umefanyika.

v. Imefanya kazi ya ujenzi wa shimo jipya (soak pit) Mombasa kwa Mchina na imezibua na kusafisha

makaro ya maji machafu katika Nyumba za Maendeleo (Michenzani bloki namba 1, 2 na 10).

vi. Imeandaa miradi mipya (3) ya Shirika ambapo michoro ya miradi hiyo tayari imeandaliwa ikiwemo mradi wa nyumba za makaazi Nyamanzi, mradi wa nyumba za makaazi na biashara Kisakasaka Unguja na mradi wa nyumba za makaazi na biashara Mfikiwa Chakechake Pemba. Pia, imefanya Uchunguzi wa Udongo (Soil Test) katika eneo la Mfikiwa, hatua zitazoendelea ni kuanza kwa ujenzi wa nyumba hizo za makaazi.

vii. Inaendelea na matengenezo ya Awamu ya pili ya Nyumba namba 1699/1705 Mkunazini Mnadani ambapo kazi hiyo ya ujenzi inafanywa na kusimamiwa na Shirika lenyewe na imefikia asilimia 40 na kazi ya kuezeka nyumba namba ZHC 19/02A-D Tibirinzi imefanyika.

viii. Imekamilisha Matengenezo ya Ofisi za Shirika Micheweni Pemba na huduma za kiofisi zimeshaanza kutolewa kwa wapangaji wa Wilaya ya Micheweni.

ix. Imefanya Uthamini wa nyumba za vijiji 34 (Nyamanzi 12 na Kisakasaka 22) zilizopo Unguja kwa ajili ya miradi mipya ya ujenzi wa nyumba za makaazi na biashara inayotarajiwa kufanyika katika maeneo hayo.

x. Imeweka vibati vya alama 582 (Unguja 455 na Pemba 127) kwa Nyumba zinazomilikiwa na Shirika zikiwemo nyumba za Maendeleo za Makunduchi (97), Mpapa (69), Gamba (137), Kikwajuni (100), Kilimani (12), Chukwani (2), K/Samaki (1), Beit el Ras (1) na Mji Mkongwe

(36) kwa Unguja na Mapinduzi (42), Ng'ombeni (2) na Mtemani (83) kwa Pemba.

xi. Imetoa Mikataba 438 (Unguja 354 na Pemba 84) ya muda mfupi kwa wapangaji wa nyumba za makaazi na milango ya biashara pamoja na Mikataba mitatu (3) ya muda mrefu kwa nyumba nam.128 A (Forodhani).

xii. Imefanya Utambuzi wa mipaka ya nyumba za Shirika kwa kushirikiana na Kamisheni ya Ardhi Pemba kwa nyumba za Police line-Wete na SMZ - Mkoani.

xiii. Imefanya Mikutano mitatu ya kuhamasisha wapangaji kulipa kodi na matumizi sahihi ya nyumba za Maendeleo Madungu (Pemba), Mpapa na Makunduchi.

xiv. Imesimamia mifumo ya ndani ya Shirika ikiwemo mfumo wa kuhifadhi taarifa za wapangaji (HMS) na kuimarisha Mfumo wa ukusanyaji mapato kupitia TEHAMA kwa kuweza kuwatumia wapangaji ankara za malipo za kila mwezi.

xv. Imewapatia Wafanyakazi 37 (34 mafunzo ya muda mfupi na 3 mafunzo ya muda mrefu) pamoja na kutayarisha Muongozo wa Mafunzo wa Shirika.

83. **Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2023/24, Programu ndogo ya Maendeleo ya Makaazi kupitia Shirika la Nyumba Zanzibar lilikadiria kukusanya jumla ya **TZS 13,446,015,000** kutoka katika vyanzo vyake vya mapato yakiwemo makusanyo ya ndani ambayo ni **TZS 3,146,015,000** sawa na **asilimia 23.3** ya makadirio

ya makusanyo, Ruzuku kutoka Serikali Kuu ni **TZS 6,800,000,000** sawa na **asilimia 50.5**. Mauzo ya nyumba za Mombasa kwa Mchina **TZS 1,500,000,000** ikiwa sawa na **asilimia 11.1** pamoja na matarajio ya Mkopo wa **TZS 2,000,000,000** sawa na **asilimia 14.8** ya makadirio yaliyopangwa.

84. **Mheshimiwa Spika;** Hadi kufikia Machi, 2024, **TZS 7,831,689,794.15** zimekusanywa sawa na **asilimia 58.1** ya makadirio. Makusanyo hayo yamejumuisha **TZS 1,790,007,591.40** kwa makusanyo ya ndani sawa na **asilimia 56.9**, **TZS 3,964,730,743.75** Mauzo ya nyumba sawa na asilimia 264 na **TZS 2,076,951,459** Ruzuku sawa na **asilimia 30.5** ya makadirio yaliyopangwa.

85. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu hii kupitia Shirika lilikadiria kutumia **TZS 13,246,487,651** kati ya fedha hizo **TZS 2,843,007,451** kwa kazi za kawaida na ulipaji mishahara na **TZS 10,403,480,200** kwa kazi za ujenzi wa miradi mipya pamoja na matengenezo ya nyumba. Hadi kufikia Machi, 2024, Shirika limetumia jumla ya **TZS 5,182,243,962** sawa na **asilimia 39.1** ya makadirio ya matumizi yaliyopangwa.

86. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Shirika la Nyumba kupitia Programu ndogo ya Maendeleo ya Makaazi itaendelea na Ujenzi wa nyumba 443 (120 za Makaazi Nyamanzi, 260 Kisakasaka, 50 Mfikiwa na nyumba 13 za Makaazi na biashara Kiembe Samaki); itaendelea na ujenzi wa (awamu ya pili) nyumba 8 za Makaazi na milango ya maduka 20 Mkungu Malofa- Chake Chake; itaendelea na mradi wa matengenezo (awamu ya pili) ya nyumba

nam. 1699/1705 Mkunazini (Mnadani); itaendelea kutafuta wawekezaji kwa lengo la kushirikiana kwenye miradi ya ujenzi wa nyumba mpya za makaazi na biashara; itaendelea kuzifanyia matengenezo nyumba za Mji Mkongwe (2) na itatafuta maeneo ya uwekezaji maeneo ya mijini pembezoni mwa barabara kwa ajili ya ujenzi wa Majengo ya Biashara.

87. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2024/25, Programu kupitia Shirika la Nyumba inatarajia kukusanya jumla ya **TZS 24,640,000,000** kutokana na kodi zake, mauzo ya nyumba, mikataba, dhamana na adhabu pamoja na mapato yanayotarajiwa kupatikana kwa kazi za ujenzi na ushauri elekezi za kampuni ya Shirika. Pia, inatarajia kuchukua mkopo wa **TZS 6,000,000,000** kutoka Benki na taasisi za fedha kwa ajili ya kuongeza Mfuko wa kazi za miradi mipya ya ujenzi inayotarajiwa kutekelezwa.

88. **Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2024/25, Programu ndogo ya Maendeleo ya Makaazi kupitia Shirika la Nyumba imekadiria kutumia jumla ya **TZS 23,594,314,868** kati ya fedha hizo **TZS 2,721,746,868** kwa kazi za kawaida na ulipaji wa mishahara na **TZS 20,871,744,000** kazi za Maendeleo.

89. **Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu Kuu PN0203 ya Maendeleo ya Makaazi kupitia Idara ya Maendeleo ya Makaazi imepangiwa kukusanya jumla ya **TZS 1,590,000,000** kutokana na vyanzo vyake vya mapato.

90. **Mheshimiwa Spika**; Ili Programu Kuu PN0203 ya Maendeleo ya Makaazi iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **TZS 40,536,432,000**

ambapo **TZS 176,532,000** Mishahara, **TZS 254,900,000** kazi za kawaida, **TZS 105,000,000** Ruzuku na **TZS 40,000,000,000** fedha za Miradi ya Maendeleo.

## MWELEKEO WA MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025.

91. **Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi imejipanga kutekeleza bajeti yake kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:

    i. Kuendelea na uandaaji wa Mipango ya matumizi ya ardhi ya Miji mbalimbali (Local Area Development Plans) Unguja na Pemba;
    ii. Kuendelea na zoezi la kufanya utambuzi wa maeneo Unguja na Pemba ili kupunguza Migogoro ya ardhi na kudhibiti ujenzi holela Nchini;
    iii. Kuanzisha Mifumo itakayotumika katika kurahisisha na kuimarisha utoaji wa huduma kwa Wananchi kupitia Sekta ya Ardhi, Nyumba na Makaazi;
    iv. Kuendelea na Ujenzi wa nyumba mpya za Makaazi na Biashara pamoja na kufanya matengenezo ya nyumba za Maendeleo na zisizokuwa za Maendeleo Unguja na Pemba;
    v. Kufanya mapitio ya Sera na Sheria za Ardhi na Makaazi ili kuimarisha ufanisi wa utekelezaji;
    vi. Kutatua migogoro ya ardhi na makaazi inayojitokeza;

vii. Kuimarisha ufanisi wa shughuli za Wizara ikiwemo kununua vifaa na kujenga uwezo wa Watendaji; na

viii. Kuimarisha na kuratibu mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa katika Sekta ya Ardhi, Nyumba na Makaazi.

92. **Mheshimiwa Spika**; Baada ya kutoa maelezo ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Mwelekeo kwa kila Programu, sasa naomba kuwasilisha mwelekeo wa Bajeti yenye kuzingatia Programu ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

93. **Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, naomba idhini ya kukusanya Mapato ya Fedha **TZS 4,270,000,000** kutoka vyanzo mbalimbali vilivyomo ndani ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi. **Kiambatanisho namba 6 (a)** kinafafanua.

94. **Mheshimiwa Spika**; Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, ili Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi iweze kutekeleza Programu Kuu na Programu Ndogo nilizozieleza, naliomba Baraza lako liidhinishe **TZS 53,062,900,000** kati ya hizo **TZS 2,613,100,000** Mishahara, **TZS 2,085,100,000** matumizi ya kawaida, **TZS 3,364,700,000** Ruzuku (**TZS 361,400,000** Ruzuku ya Matumizi Mengineyo na **TZS 3,003,300,000** ni Ruzuku ya Mishahara) na **TZS 45,000,000,000** kwa kutekeleza Miradi ya Maendeleo. **Kiambatanisho namba 6 (b)** kinafafanua.

95 **Mheshimiwa Spika**; Kwa upande wa matumizi ya Kamisheni ya Ardhi, naliomba Baraza lako kuidhinisha matumizi ya asilimia 50 yatokanayo na Makusanyo ya Kamisheni ya Ardhi (Retention).

## HITIMISHO

96. **Mheshimiwa Spika;** Baada ya uwasilishaji huo, sasa nachukua fursa hii kwa mara nyengine tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uwezo wa kuisoma Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

97. **Mheshimiwa Spika**; Vilevile, naomba kumshukuru tena Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa kuendelea kuwa na imani kwangu ya kunipa nafasi hii muhimu ya kuitumikia Nchi yangu kupitia Wizara hii, nami naahidi kuendelea kujitahidi kadri ya uwezo wangu wote kumsaidia katika kuwaletea Maendeleo Wananchi.

98. **Mheshimiwa Spika**; Kwa mara nyengine tena naomba kukushukuru wewe mwenyewe, Naibu Spika, Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati, Makamo Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe wote kwa kunisikiliza kwa utulivu na kwa umakini mkubwa wakati nikisoma Hotuba ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi. Pia, napenda kuwashukuru Washirika wote wa Maendeleo walioshirikiana nasi katika kutekeleza majukumu yetu wakiwemo "Taasisi ya kushughulikia taarifa za Kijiografia na Misitu ya Nchini Ufaransa

(Institue of Geographic and Forest Information -IGNFI), Benki ya Dunia, European Union, Jamhuri ya Watu wa China na Regional Center for Mapping of Resources for Development. Aidha, nazishukuru Benki zote zilizoonesha nia ya kuwekeza katika Sekta ya Ardhi, Nyumba na Makaazi ikiwemo Benki ya Watu ya Zanzibar (PBZ), NMB, BPI na CRDB.

99. **Mheshimiwa Spika;** Navishukuru vyombo vyote vya habari vilivyoshirikiana nasi katika kuelimisha jamii juu ya shughuli zinazofanywa na jamii vikiwemo ZBC TV na Redio, TBC TV na redio, Tifu TV, Azam TV, ZCTV, Zanzibar TV, ITV, STAR TV, Channel 10 TV na Gazeti la Zanzibar leo. Aidha, Sitaweza kuwataja Wadau wote lakini naomba Wadau wote wa Sekta Binafsi na Washirika wa Maendeleo walioshirikiana nasi wapokee Shukrani zetu za dhati na tunawaomba waendelee kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Zanzibar.

100. **Mheshimiwa Spika**; Shukurani za pekee kabisa ziwaendee wafanyakazi wote wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Unguja na Pemba kwa Ushirikiano wao mkubwa kwangu walionionesha, namuomba Mwenyezi Mungu awajaalie wote afya njema na maisha marefu yenye kheri na baraka. Naamini ushirikiano huo utaendelea ili tuweze kuendelea kutoa huduma bora kwa Wananchi.

101. **Mheshimiwa Spika**; Natoa shukrani zangu za pekee kwa Uongozi wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi tukianzia na Naibu Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Mheshimiwa Salha Mohammed Mwinjuma;

Katibu Mkuu Ndugu Khadija Khamis Rajab; Naibu Katibu Mkuu Ndugu, Mhaza Gharib Juma; Afisa Mdhamini Pemba Ndugu Bakari Ali Bakari, Wakurugenzi wote, Wakuu wa Taasisi, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi zote zilizo chini ya Wizara, Washauri wa Mahakama ya Ardhi Unguja na Pemba pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mashirikiano wanayonipa katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku. Nawaomba waendelee kuendeleza mshikamano huu ili tuweze kuwaletea wananchi maendeleo endelevu kupitia Sekta ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi.

102. **Mheshimiwa Spika**; Nachukua fursa hii kuwashukuru Wadau mbalimbali wa Serikali walioshirikiana nasi kwa karibu ikiwemo Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Uratibu na Baraza la Wawakilishi; Ofisi ya Rais – Ikulu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalamu za SMZ; Ofisi ya Rais Fedha na Mipango; Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora; Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo; Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi; Wizara Kilimo Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo; Wizara ya Maji, Nishati na Madini; Wakuu wa Mikoa; Wakuu wa Wilaya; Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGAs); ZIPA; Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA); Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali; Taasisi za Fedha; Masheha pamoja na Wananchi kwa ushirikiano mkubwa wanaoutoa kwa Wizara katika kuhakikisha kuwa majukumu tuliopewa yanatekelezwa kama yalivyokusudiwa na kwa ufanisi mkubwa.

103. **Mheshimiwa Spika**; Vile vile, napenda kuishukuru Afisi ya Rais Ufuatiliaji na Utendaji Kazi Serikalini (PDB) kwa mashirikiano yao wanayotupa katika kusimamia utekelezaji wa Miradi ya Wizara ikiwemo Mradi wa Usajili wa Ardhi (LARIS) pamoja na Taasisi ya SEMA na Rais (SNR) kwa kushirikiana katika kufuatilia na kutatua changamoto mbali mbali zinazojitokeza zinazotokana na huduma zinazotolewa na Wizara.

104. **Mheshimiwa Spika**; Mwisho kabisa, napenda kuishukuru familia yangu kwa upendo wao, michango, uvumilivu, subira na ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kutekeleza majukumu makubwa ya Kitaifa niliyokabidhiwa. Shukrani za pekee ziende kwa Mume wangu Mpenzi na kwa namna ya pekee kabisa nawashukuru Kinamama wa Mkoa wa Kusini Unguja kwa kunipa ushirikiano wao mkubwa na kuunga mkono juhudi mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali za kuwaletea Wananchi Maendeleo.

105**. Mheshimiwa Spika**; nawaomba sasa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako waipokee, waijadili kwa kina Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kisha watushauri na kutuelekeza na hatimae wayapitishe makadirio haya. Tuna imani kubwa kuwa michango ya Waheshimiwa Wajumbe itatusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu ya kazi vizuri zaidi katika kipindi kijacho cha Mwaka wa Fedha 2024/2025.

106. **Mheshimiwa Spika**; Naomba kutoa hoja.



……………………………………………..

**MHESHIMIWA RAHMA KASSIM ALI (MBM)**
**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI**
**ZANZIBAR.**

**KIAMBATANISHO NAM: 1(a)**

**MUHTASARI WA UKUSANYAJI WA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024**

| PROGRAMU KUU | PROGRAMU NDOGO/ HUDUMA | KASMA | CHANZO CHA MAPATO | FEDHA ILIYOPANGWA KUKUSANYWA KWA MWAKA | MAKADIRIO YA MIEZI TISA JULAI 2022 HADI MACHI 2023 | FEDHA ILIYOKUSANYWA JULAI 2023 – MACHI 2024 | ASILIMIA YA MAKADIRIO YA MIEZI TISA | ASILIMIA YA MAKADIRIO YAMWAKA 2022/2023 | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **UTAWALA NA UENDESHAJI** | Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba | 1422070 | Ada ya Mahakama | 7,000,000 | 5,160,000 | 2,839,400 | **55** | **41** | |
| | | 1422008 | Vibali vya Ujenzi | 21,000,000 | 14,900,000 | 9,460,000 | **63** | **45** | Mapato yanakusanywa na Halmashauri na uhaba wa vitendea kazi vya ufuatiliaji |
| | | **Jumla ndogo** | | **28,000,000** | **20,060,000** | **12,289,400** | **61** | **44** | |
| | | | | | | | | | |
| | Uratibu wa Mipango Sera na Utafiti | 1422008 | Ada ya Vibali vya Ujenzi | 1,476,000,000 | 1,104,500,000 | 449,676,401 | **41** | **30** | |
| | | **Jumla ndogo** | | 1,476,000,000 | 1,104,500,000 | 449,676,401 | **41** | **30** | |
| | **JUMLA KUU** | | | **1,504,000,000** | **1,124,560,000** | **461,965,801** | **41** | **31** | |
| | | | | | | | | | |
| **USIMAMIZI WA ARDHI** | Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi | 1422072 | Ada ya Mahakama | 10,000,000 | 7,450,000 | 6,133,821 | **82** | **61** | |
| | Kusimamia na Kuidhinisha Ripoti za Uthamini | 1422093 | Ada ya Uthamini | 270,000,000 | 201,800,000 | 104,871,324 | **51** | **39** | Taasisi za Serikali baadhi hazilipii ada ya uthamini |
| | | | | **280,000,000** | **209,250,000** | **111,005,145** | **53** | **40** | |
| | | | | | | | | | |
| | Upangaji na Usimamizi wa Ardhi | 1422008 | Nyaraka za Ardhi | 481,584,000 | 123,815,230 | 898,036,476 | **725** | **186** | Kuimarika kwa mifumo na kushajihika kwa wananchi kusajili ardhi na kuimarika kwa Sekta ya Uwekezaji |
| | | 1422028 | Muongozo wa matumizi ya ardhi | 60,041,000 | 16,291,000 | 82,741,864 | **508** | **138** | |
| | | 1422043 | Upimaji na Ramani | 526,616,000 | 139,080,000 | 523,202,583 | **376** | **99** | |
| | | 1422074 | Usajili wa Ardhi | 90,094,000 | 23,022,000 | 48,666,181 | **211** | **54** | |
| | | 1422093 | Uthamini | 92,555,000 | 24,900,000 | 53,508,000 | **215** | **58** | |
| | | 1422090 | Uhaulishaji | 1,500,000,000 | 438,000,000 | 3,226,426,960 | **737** | **215** | |
| | | **Jumla ndogo** | | **2,750,890,000** | **765,108,230** | **4,832,582,064** | **632** | **176** | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **MAENDELEO YA MAKAAZI** | Usajili wa Majengo na Jumuia za Kondominio | 1422119 | Ada ya usajili wa Kondominio | 350,000,000 | 256,000,000 | 526,191,036 | **206** | **150** | Kuimarika uwekezaji katika sekta ya milki na kufanya ukaguzi na kushajihisha na wananchi wa nyumba za maendeleo |
| | | **Jumla ndogo** | | **350,000,000** | **256,000,000** | **526,191,036** | **206** | **150** | |
| | | | | | | | | | |
| | BODI YA USAJILI WAKANDARASI | 1500009 | Ada ya usajili Wakandarasi | 1,657,713,000 | 1,173,510,500 | 670,093,500 | **57** | **40** | |
| | BODI YA USAJILI WASANIFU | 1112006 | Ada ya usajili Wahandisi | 527,000,000 | 401,385,000 | 413,196,000 | **103** | **78** | |
| | | **Jumla ndogo** | | **2,184,713,000** | **1,574,895,500** | **1,083,289,500** | | | |
| **JUMLA** | | | | **7,069,603,000** | **3,929,813,730** | **7,015,033,546** | **179** | **99** | |
| | ***WAKALA WA MAJENGO ZANZIBAR** | | | 436,000,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | |
| | **JUMLA KUU** | | | **7,505,603,000** | **7,094,519,230** | **7,015,033,546** | **99** | **93** | |

**KIAMBATANISHO NAM 1(b).**

## MUHTASARI WA MATUMIZI YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

| MUHTASARI | KWA MWAKA 2023/2024 | MAKADIRIO JULAI 2023 HADI MARCH 2024 | MATUMIZI JULAI 2023 HADI MARCH 2024 | ASILIMIA JULAI 2023 HADI MACHI 2024 | ASILIMIA YA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|
| MISHAHARA | 7,120,224,000 | 5,339,626,317 | 4,550,921,975 | 85 | 64 |
| MATUMIZI MENGINEYO | 3,340,281,000 | 2,560,541,086 | 1,430,226,921 | 56 | 20 |
| RUZUKU YA MATUMIZI (OC) | 986,075,000 | 960,936,970 | 273,196,000 | 28 | 28 |
| MIRADI YA MAENDELEO SMZ | 4,550,000,000 | 4,082,400,000 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA NDOGO** | **15,996,580,000** | **12,943,504,373** | **6,254,344,896** | **48** | **39** |
| -WAKALA WA MAJENGO<br>-BODI YA USAJILI WAHANDISI<br>-BODI YA WAKANDARASI | 1,012,620,000 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA KUU** | **17,009,200,000** | **12,943,504,373** | **6,254,344,896** | **48** | **36** |

**KIAMBATANISHO NAM 1(c).**

## MCHANGANUO WA MAKADIRIO YA BAJETI KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

| PROGRAM | MAKISIO KWA MWAKA 2023/2024 | MAKISIO MATUMIZI YA MSHAHARA KWA MWAKA 2023/2024 | MAKISIO MATUMIZI YA OC KWA MWAKA 2023/2024 | MAKISIO MATUMIZI YA RUZUKU KWA MWAKA 2023/2024 | MAKISIO MATUMIZI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2023/2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| **UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA** | | | | | |
| Uratibu wa Mipango Sera na Utafiti | 744,430,000 | 187,412,000 | 557,018,000 | 0 | 0 |
| Utawala na Uendeshaji | 3,149,062,000 | 2,744,061,000 | 405,001,000 | 0 | 0 |
| Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba | 1,054,004,000 | 805,423,000 | 248,581,000 | 0 | 0 |
| **Jumla Ndogo** | **4,947,496,000** | **3,736,896,000** | **1,210,600,000** | **0** | **0** |
| | | | | | |
| **USIMAMIZI WA ARDHI** | | | | | |
| Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi | 587,604,000 | 342,604,000 | 245,000,000 | | |
| Kusimamia na Kuidhinisha Ripoti za Uthamini | 213,680,000 | 0 | 0 | 213,680,000 | |
| **Jumla Ndogo** | **801,284,000** | **342,604,000** | **245,000,000** | **213,680,000** | |
| Upangaji na Usimamizi wa Ardhi | 9,985,300,000 | 3,040,724,000 | 1,621,500,040 | 773,075,960 | 4,550,000,000 |
| **Jumla Ndogo** | **9,985,300,000** | **3,040,724,000** | **1,621,500,040** | **773,075,960** | **4,550,000,000** |
| | | | | | |
| **MAENDELEO YA MAKAAZI** | | | | | |
| Usajili wa Majengo na Jumuia za Kondominio | 168,000,000 | 0 | 0 | 168,000,000 | 0 |
| Utatuzi wa Migogoro kwa Wapangaji wa Nyumba | 94,500,000 | 0 | 0 | 94,500,000 | 0 |
| **Jumla Ndogo** | **262,500,000** | **0** | **0** | **262,500,000** | **0** |
| **JUMLA KUU** | **15,996,580,000** | **7,120,224,000** | **3,077,100,040** | **1,249,255,960** | **4,550,000,000** |

**KIAMBATANISHO NAM 1(d).**

**MCHANGANUO WA MAKADIRIO YA BAJETI KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI 2023- MACHI 2024)**

| | MAKISIO KWA MIEZI TISA JULAI 2023 HADI MACHI 2024 | MAKISIO MATUMIZI YA OC JULAI 2023 HADI MACHI 2024 | MAKISIO MATUMIZI YA MSHAHARA JULAI 2023 HADI MACHI 2024 | MAKISIO MATUMIZI YA RUZUKU YA OC JULAI 2023 HADI MACHI 2024 | MAKISIO MATUMIZI YA MAENDELEO JULAI 2023 HADI MACHI 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| **UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI** | | | | | |
| Uratibu wa Mipango Sera na Utafiti | 587,721,787 | 447,162,700 | 140,559,087 | 0 | 0 |
| Utawala na Uendeshaji | 2,369,592,550 | 311,546,800 | 2,058,045,750 | 0 | 0 |
| Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba | 819,353,640 | 215,285,700 | 604,067,940 | 0 | 0 |
| **Jumla Ndogo** | **3,776,667,977** | **973,995,200** | **2,802,672,777** | **0** | **0** |
| | | | | | |
| **USIMAMIZI WA ARDHI** | | | | | |
| Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi | 440,703,540 | 183,750,000 | 256,953,540 | 0 | 0 |
| Kusimamia na Kuidhinisha Ripoti za Uthamini | 164,755,000 | 0 | 0 | 164,755,000 | 0 |
| **Jumla Ndogo** | **605,458,540** | **183,750,000** | **256,953,540** | **164,755,000** | **0** |
| Upangaji na Usimamizi wa Ardhi | 4,262,606,856 | 1,402,795,886 | 2,280,000,000 | 579,806,970 | 4,082,400,000 |
| **Jumla Ndogo** | **4,262,606,856** | **1,402,795,886** | **2,280,000,000** | **579,806,970** | **4,082,400,000** |
| | **4,868,065,396** | **1,586,545,886** | **2,536,953,540** | **744,561,970** | **4,082,400,000** |
| | | | | | |
| **MAENDELEO YA MAKAAZI** | | | | | |
| Usajili wa Majengo na Jumuia za Kondominio | 135,000,000 | 0 | 0 | 135,000,000 | 0 |
| Utatuzi wa Migogoro kwa Wapangaji wa Nyumba | 81,375,000 | 0 | 0 | 81,375,000 | 0 |
| **Jumla Ndogo** | **216,375,000** | **0** | **0** | **216,375,000** | **0** |
| **JUMLA KUU** | **8,861,108,373** | **2,560,541,086** | **5,339,626,317** | **960,936,970** | **4,082,400,000** |

**KIAMBATANISHO NAM 1(e).**

**MUHTASARI WA MATUMIZI YA BAJETI KWA PROGRAMU KUU NA NDOGO KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 – MACHI 2024**

| PROGRAMU KUU | PROGRAMU NDOGO/ HUDUMA | MAKISIO KWA MWAKA 2023/2024 | MAKISIO KWA ROBO 3 | KILICHOPATIKANA JULAI 2023- MACHI 2024 | MISHAHARA NA POSHO | MATUMIZI MENGINEYO | MATUMIZI YA RUZUKU YA OC | MATUMIZI FEDHA ZA MAENDELEO | ASILIMIA ROBO TATU | ASILIMI A MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi | Uratibu wa Mipango Sera na Utafiti | 744,430,000 | 587,721,787 | 291,326,835 | 162,796,840 | 128,529,995 | 0 | 0 | **50** | **39** |
| | Utawala na Uendeshaji | 3,149,062,000 | 2,369,592,550 | 1,562,016,994 | 1,366,245,631 | 195,771,363 | 0 | 0 | **66** | **50** |
| | Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba | 1,054,004,000 | 819,353,640 | 615,302,101 | 527,662,101 | 87,640,000 | 0 | 0 | **75** | **58** |
| | **Jumla ndogo** | **4,947,496,000** | **3,933,376,190** | **2,468,645,930** | **2,056,704,572** | **411,941,358** | **0** | **0** | **63** | **50** |
| Usimamizi wa Ardhi | Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi | 587,604,000 | 455,383,540 | 342,410,689 | 268,712,047 | 73,698,642 | **0** | **0** | **75** | **58** |
| | Kusimamia na Kuidhinisha Ripoti za Uthamini | 213,680,000 | 164,755,000 | 77,023,000 | 0 | 0 | 77,023,000 | **0** | **47** | **36** |
| | **Jumla ndogo** | **801,284,000** | **620,138,540** | **419,433,689** | **268,712,047** | **73,698,642** | **77,023,000** | **0** | **68** | **52** |
| | Upangaji na Usimamizi wa Ardhi | 9,985,300,000 | 4,262,606,856 | 3,264,514,356 | 2,225,505,356 | 944,586,000 | 94,423,000 | 0 | **77** | **33** |
| | **Jumla ndogo** | **9,985,300,000** | **4,262,606,856** | **3,264,514,356** | **2,225,505,356** | **944,586,000** | **94,423,000** | **0** | **77** | **33** |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Maendeleo ya Makaazi | Usajili wa Majengo na Jumuia za Kondominio | 168,000,000 | 135,000,000 | 61,835,000 | 0 | 0 | 61,835,000 | 0 | **46** | **37** |
| | Utatuzi wa Migogoro kwa Wapangaji wa Nyumba | 94,500,000 | 81,375,000 | 39,915,000 | 0 | 0 | 39,915,000 | 0 | **49** | **42** |
| | **Jumla ndogo** | **262,500,000** | **216,375,000** | **101,750,000** | **0** | **0** | **101,750,000** | **0** | **47** | **39** |
| | **JUMLA KUU** | **15,996,580,000** | **9,032,496,586** | **6,254,343,975** | **4,550,921,975** | **1,430,226,000** | **273,196,000** | **0** | **69** | **39** |

**KIAMBATANISHO "NO 2"**

**MAENEO YALIYOFANYIWA UKAGUZI WA UJENZI**

| SN | WILAYA | ENEO |
|---|---|---|
| 1. | Wilaya ya Kati | Uroa, Mwea Pongwe, Jumbi, Chwaka, Kikungwi, Tunguu na Ubago |
| 2. | Wilaya ya Kusini | Michamvi, Bwejuu, Paje Makunduchi na Jambiani |
| 3. | Wilaya ya Magharib A | Mbuzini, Kianga, Chuini, Mwera, Mwakaje, Kijichi na Masingini |
| 4. | Wilaya ya Magharib B | Fuoni Uwandani, Fuoni Mambosasa, Taveta, Kijitoupele, Bweleo, Dimani, Tomondo, Kombeni, Chukwani, Kibondemzungu, Kisauni, Fuoni Chunga, Mbweni, Shakani, Buyu, Maungani, Kisakasaka, Jitimai, Kiembesamaki, Fuoni Kibondeni na Michungwani |
| 5. | Wilaya ya Kaskani A | Nungwi, Matemwe na Pwani Mchangani |
| 6. | Wilaya ya Kaskazini B | Kiwengwa, Kwa Gube, Kitope na Fujoni |
| 7. | Kusini Pemba | Chakechake na Mkoani |
| 8. | Kaskazini Pemba | Michweni na Wete |

**KIAMBATANISHO NAMBARI 3:**

**IDADI YA WAFANYAKAZI WALIOPATIWA LIKIZO NA STAHIKI**

| NAM. | AINA YA STAHIKI | WANAUME | WANAWAKE | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | LIKIZO | 7 | 7 | **14** |
| 2. | MALIPO YA MUDA WA ZIADA | 5 | 4 | **9** |
| 3. | UBANI | 3 | - | **3** |
| 4. | TATHMINI YA UTENDAJI KAZI | 16 | 15 | **31** |
| | **JUMLA** | **31** | **26** | **57** |

**KIAMBATISHO NAMBARI:4 (a)**

**MAFUNZO YA MUDA MFUPI KWA WAFANYAKAZI WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024**

| S/N | TAASISI/IDARA | WANAUME | | WANAWAKE | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | NDANI YA NCHI | NJE YA NCHI | NDANI YA NCHI | NJE YA NCHI | |
| 1. | UENDESHAJI NA UTUMISHI | 18 | 0 | 29 | - | **47** |
| 2. | MIPANGO SERA NA UTAFITI | 1 | 0 | 0 | - | **1** |
| 3. | MAHAKAMA YA ARDHI | 5 | 0 | 13 | - | **18** |
| 4. | SHIRIKA LA NYUMBA | 26 | 1 | 18 | - | **45** |
| 5. | OFISI YA MTHAMINI MKUU | 4 | 0 | 8 | - | **12** |
| 6. | KAMISHENI YA ARDHI | 19 | 0 | 14 | - | **33** |
| | **JUMLA KUU** | 73 | 1 | 82 | - | **156** |

**KIAMBATANISHO NAMBARI 4 (b)**

**MAFUNZO YA MUDA MREFU KWA WAFANYAKAZI WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI 2023/2024.**

| - | AINA YA MAFUNZO | WANAUMEME | WANAWAKE | JUMLA | CHUO | MWAKA WA KUMALIZA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI | DEGREE IN MASS COMMUNICATION | 0 | 1 | 1 | OPEN UNIVERSITY OT TANZANIA (OUT) | 2025 |
| | MASTER IN BUSINESS ADMINISTRATION | 0 | 1 | 1 | OPEN UNIVERSITY | 2025 |
| | MASTERS IN INFORMATION SECURITY | 1 | 0 | 1 | ARDHI UNIVERTY - DAR ES SALAM | 2025 |
| | MASTERS IN SOFTWARE ENGINEERING | 1 | 0 | 1 | NANKAI UNIVERSITY CHINA | 2025 |
| AFISI KUU PEMBA | DEGREE IN HUMAN RESOURCE MGNT | 0 | 1 | 1 | INSTITUTE OF PUBLIC ADMINISTRATION | 2024 |
| | DIPLOMA IN RECORDING AND ARCHIVE MANAGEMENT | 0 | 2 | 2 | INSTITUTE OF PROFFESIONAL AND INNOVATION DEVELOPMET | 2024 |
| | DIPLOMA IN ECONOMY DEVELOPMENT | 0 | 1 | 1 | MWALIMU NYERERE MOMORIAL ACADEMY | 2024 |
| | MASTER IN BUSENESS ADMINISTRATION | 0 | 1 | 1 | BEJIN INTERNATIONAL STUDIES UNIVERSITY | 2024 |
| MAHAKAMA YA ARDHI | DEGREE IN LAW | 0 | 2 | 2 | OPEN UNIVERSITY | 2025 |
| | DEGREE IN LAW | 0 | 1 | 1 | ZANZIBAR UNIVERSITY | 2024 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| SHIRIKA LA NYUMBA | PhD IN ECONOMICS | 1 | 0 | 1 | POLTOVA UNIVERSITY OF ECONOMICS (UKRAINE) | 2024 |
| | DEGREE IN ARCHITECTURE | 0 | 1 | 1 | ARDHI UNIVERSITY | 2026 |
| | CERTIFICATE IN SECRETARY | 0 | 1 | 1 | IPA | 2025 |
| MTHAMINI MKUU WA SERIKALI | PhD IN DEVELOPMENT STUDY | 0 | 1 | 1 | TOYO UNIVERSITY-JAPAN | 2026 |
| | PROCUREMENT AND SUPPLY | 1 | 0 | 1 | ICPS | 2026 |
| | CERTIFICATE HRM | 0 | 1 | 1 | IPA | 2026 |
| | CERTIFICATE HRM | 0 | 1 | 1 | OPEN UNIVERSITY | 2025 |
| KAMISHENI YA ARDHI | PRE-STUDIES | 0 | 1 | 1 | KIU | 2028 |
| | SOCIAL AND ECONOMIC DEV. | 1 | 0 | 1 | MWL.NYERERE | 2025 |
| | CIVIL AND TRANS.ENGENEER | 0 | 1 | 1 | KARUME | 2025 |
| | BUSINESS ADMINISTRATION | 1 | 0 | 1 | ZU | 2025 |
| | URBAN PLANNING | 0 | 1 | 1 | ARDHI UNIVERSITY DERESALAM | 2025 |
| | MANAGEMENT AND SOCIAL DEVELOPMENT | 0 | 1 | 1 | MWALIM NYERERE - ZNZ | 2025 |
| | MANAGEMENT AND SOCIAL DEVELOPMENT | 0 | 1 | 1 | MWALIM NYERERE - ZNZ | 2026 |
| | SOCIAL AND ECONOMIC DEV. | 0 | 1 | 1 | MWALIM NYERERE - ZNZ | 2025 |
| | DATA SCIEN.AND ARTIFICIAL INTELIGENCE | 1 | 0 | 1 | INDIA UNIVERSITY OF MADRAS | 2026 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | INFORMATION AND OFFICE MNG. | 0 | 1 | 1 | ZU | 2025 |
| | PHD IN DESIGN AND ARCHITECTURE | 1 | 0 | 1 | ALTO UNIVERSITY - FINLAND | 2025 |
| KAMISHENI YA ARDHI - PEMBA | MASTER OF LAW IN LAND ADMINISTRATION AND MANAGEMENT | 1 | 0 | 1 | OPEN UNIVERSITY | 2025 |
| | DEGREE IN LAND MANAGEMENT AND VALUATION | 1 | 0 | 1 | ARDHI UNIVERSITY | 2024 |
| | DEGREE IN URBAN PLANNING | 1 | 0 | 1 | ARDHI UNIVERSTY | 2024 |
| | DEGREE IN MASS COMMUNICATION | 1 | 0 | 1 | OPEN UNIVERSITY | 2024 |
| **JUMLA** | | **12** | **22** | **34** | | |

**KIAMBATISHO 5:**

**MASHAURI MAPYA YALIYOPOKELEWA, YANAYOENDELEA MAHAKAMANI PAMOJA NA YALIYOTELEWA UAMUZI KWA KIPINDI CHA KUTOKA JULAI 2023 HADI MACHI, 2024.**

| MKOA HUSIKA | KESI MPYA ZILIZOPOKELEWA | KESI ZILIZOTOLEWA MAAMUZI | KESI ZINAZOENDELEA MAHAKAMANI |
|---|---|---|---|
| Mjini Magaharibi | 41 | 27 | 85 |
| Kaskazini Unguja | 15 | 15 | 34 |
| Kusini Unguja | 27 | 16 | 34 |
| Kaskazini Pemba | 23 | 20 | 25 |
| Kusini Pemba | 29 | 30 | 40 |
| **JUMLA KUU** | **135** | **108** | **218** |

**KIAMBATANISHO NAMBARI: 6(a)**

**MAKADIRIO YA UKUSANYAJI WA MAPATO KWA FUNGU LA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

| TAASISI | KASMA | CHANZO CHA MAPATO | FEDHA INAYOPANGWA KUKUSANYWA |
|---|---|---|---|
| **PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI -PN0201** | | | |
| OFISI KUU PEMBA | 1422016 | Ada ya Vibali vya Ujenzi (DCU) | 36,000,000 |
| | 1422070 | Ada ya Mahakama | 7,000,000 |
| | **Jumla ndogo** | | **43,000,000** |
| IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI | 1422016 | Ada ya Vibali vya Ujenzi (DCU) | 2,127,000,000 |
| **Jumla ndogo** | | | **2,170,000,000** |
| | | | |
| **PROGRAMU YA USIMAMIZI WA ARDHI -PN0202** | | | |
| OFISI YA MTHAMINI MKUU WA SERIKALI | 1422093 | Ada ya Uthamini | 500,000,000 |
| MAHAKAMA YA ARDHI | 1422070 | Ada ya Mahakama | 10,000,000 |
| **Jumla ndogo** | | | **510,000,000** |
| **PROGRAMU YA MAENDELEO YA MAKAAZI – PN0203** | | | |
| IDARA YA MAENDELEO YA MAKAAZI | 1422119 | Ada ya usajili wa Kondominio | 1,590,000,000 |
| **Jumla ndogo** | | | **1,590,000,000** |
| **JUMLA KUU** | | | **4,270,000,000** |

**KIAMBATANISHO NAMBARI: 6(b)**

**MAKADIRIO YA FEDHA ZA MATUMIZI KWA FUNGU LA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

| PROGRAMU KUU | PROGRAMU NDOGO/ HUDUMA | TAASISI/ IDARA | MAKISIO KWA MWAKA 2024/2025 | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | MATUMIZI MENGINEYO | MISHAHARA | RUZUKU | KAZI ZA MEANDELEO | JUMLA YA FEDHA ILIYOPANGWA |
| Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi | Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti | Idara ya Mipango ,Sera na Utafiti | 600,000,000 | 236,498,000 | - | 5,000,000,000 | 5,836,498,000 |
| | Utawala na Uendeshaji | Idara ya Uendeshaji na Utumishi | 405,000,000 | 1,416,535,000 | - | - | 1,821,535,000 |
| | Uratibu na utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba | Afisi Kuu Pemba | 445,100,000 | 419,836,000 | - | - | 864,936,000 |
| | **Jumla ndogo** | | **1,450,100,000** | **2,072,869,000** | **-** | **-** | **8,522,969,000** |
| Usimamizi wa Ardhi | Kusimamia na Kuidhinisha Ripoti za Uthamini | Afisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali | - | - | 256,400,000 | - | 256,400,000 |
| | Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi | Mahakama ya Ardhi | 380,100,000 | 363,699,000 | - | - | 743,799,000 |
| | Upangaji na Usimamizi wa Ardhi | Kamisheni ya Ardhi | - | - | 3,003,300,000 | - | 3,003,300,000 |
| | **Jumla Ndogo** | | **380,100,000** | **363,699,000** | **3,364,700,000** | **-** | **4,003,499,000** |
| Maendeleo ya Makaazi | Kuboresha Upatikanaji wa Nyumba za Kisasa na za bei Nafuu Nchini | Idara ya Maendeleo ya Makaazi | 254,900,000 | 176,532,000 | - | 40,000,000,000 | 40,431,432,000 |
| | Utatuzi wa Migogoro kwa Wapangaji wa Nyumba | Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba | - | - | 105,000,000 | - | 105,000,000 |
| | **Jumla ndogo** | | **254,900,000** | **176,532,000** | **105,000,000** | **40,000,000,000** | **40,536,432,000** |
| **JUMLA KUU** | | | **2,085,100,000** | **2,613,100,000** | **3,364,700,000** | **45,000,000,000** | **53,062,900,000** |